Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# TAKWIMU ZA HALI YA UHALIFU NA MATUKIO YA USALAMA BARABARANI JANUARI – DESEMBA 2020


**Jeshi la Polisi Tanzania**
**Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**
**Dodoma**

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**
**Wizara ya Fedha na Mipango**
**Dodoma**


**Januari 2021**

***DIRA***

*Kuwa jeshi lenye weledi katika kudumisha usalama wa watu na mali zao katika jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

***DHIMA***

*Kutoa huduma bora zitakazwezesha kubaini, kuzuia na kudhibiti uhalifu katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania*

***DHAMIRA***

***Weledi***

*Kufanya kazi kwa kujitoa, Nidhamu na kuwa na matarajio.*

***Uzalendo***

*Kuwa jasiri, Mwaminifu na Mtiifu kwa nchi*

***Uadilifu***

*Kuwa Mwaminifu, Kutokuwa na upendeleo na ubadhirifu*

***Ubunifu***

*Kuwa mdadisi, Mbunifu, kufanyakazi kwa ufanisi na kujifunza*

***Hshima***

*Kufanya kazi kwa kuheshimiana, kuwa na Umoja upendo na Amani*

Imetayarishwa na

Inspekta Jenerali wa Polisi,
Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Tanzania,
S.L.P. 961,
Dodoma.

Simu: +255 (026) 232385
Nukushi: +255 (026) 232386
Tovuti: www.policeforce.go.tz

## YALIYOMO

Orodha ya Majedwali ... iv
Orodha ya Michoro ... vii
DIBAJI ... viii
MAANA YA VIFUPISHO ... x
MUHTASARI ... xi
SURA YA KWANZA ... 1
USULI ... 1
1.0 Utangulizi ... 1
1.1 Jiografia na Utawala ... 1
1.2 Jeshi la Polisi Tanzania ... 2
1.2.1 Majukumu ya Jeshi la Polisi ... 2
1.2.2 Takwimu za Jeshi la Polisi ... 2
1.2.3 Kitengo cha Takwimu cha Jeshi la Polisi ... 3
SURA YA PILI ... 4
HALI YA UHALIFU NCHINI ... 4
2.0 Utangulizi ... 4
2.1 Takwimu za Uhalifu Tanzania ... 4
2.2 Uchambuzi wa Makosa Makubwa ya Jinai ... 8
2.2.1 Makosa Dhidi ya Binadamu ... 8
2.2.2 Makosa ya Kuwania Mali ... 9
2.2.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii ... 10
2.3 Uchambuzi wa Makosa Makubwa ya Jinai kwa Mikoa ya Kipolisi ... 10
2.3.1 Makosa Dhidi ya Binadamu ... 10
2.3.2 Makosa ya Kuwania Mali ... 12
2.3.3 Makosa ya Uhalifu wa Kifedha ... 13
2.3.4 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii ... 14
2.4 Uchambuzi wa Makosa Madogo ya Jinai kwa Mkoa wa Kipolisi ... 16
2.5 Matukio yenye Athari Kubwa katika Jamii ... 18
2.5.1 Mauaji na Sababu Zake ... 18
2.5.2 Migogoro ya Ardhi ... 20
2.5.3 Makosa ya Ukatili wa Kijinsia na Unyanyasaji ... 21
2.5.4 Makosa ya Ukatili wa Kijinsia kwa Watoto ... 24
2.5.5 Makosa ya Ukatili wa Kijinsia kwa Watu wazima ... 27
2.5.6 Makosa ya Kupatikana na Silaha ... 30
2.5.7 Matukio ya Uhalifu Yaliyotendwa na Raia wa Kigeni Hapa Nchini ... 32
2.5.8 Matukio ya Uhalifu Waliotendewa Raia wa Kigeni Hapa Nchini ... 32
2.5.9 Uhamiaji Haramu ... 34
2.5.10 Matukio ya Uhalifu kwa Njia ya Mtandao ... 36

2.5.11 Matukio ya Uhalifu wa Dawa za Kulevya ... 36
2.5.12 Matukio ya Kujichukulia Sheria Mkononi ... 40
2.6 Matukio ya Shule Kuungua Moto ... 41
2.7 Matukio Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ... 42
2.8 Namna Kesi Zilivyoshughulikiwa ... 45
SURA YA TATU ... 48
USALAMA BARABARANI ... 48
3.0 Utangulizi ... 48
3.1 Makosa ya Usalama Barabarani katika Mikoa ya Kipolisi ... 48
3.1.1 Hali na Mwelekeo wa Usalama Barabarani Nchini. ... 50
3.2 Ajali za Pikipiki ... 52
3.3 Vyanzo vya Ajali za Barabarani Tanzania Bara ... 55
SURA YA NNE ... 57
MWELEKEO WA HALI YA UHALIFU ... 57
4.0 Utangulizi ... 57
4.1 Mwelekeo wa Makosa ya Jinai ... 57
4.2 Mwelekeo wa Makosa ya Usalama Barabarani ... 60
SURA YA TANO ... 61
OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA ... 61
5.0 Utangulizi ... 61
5.1 Majalada Yaliyopokelewa na Kufanyiwa Kazi ... 61
5.2 Uendeshaji wa Kesi za Jinai ... 62
5.3 Ukamilishaji wa Kesi za Jinai ... 64
5.4 Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Upelelezi ... 65
SURA YA SITA ... 66
TAARIFA YA WAFUNGWA WALIOPOKELEWA MAGEREZANI NA WALIONUFAIKA NA MSAMAHA WA RAIS ... 66
6.0 Utangulizi ... 66
6.1 Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani ... 66
6.2 Wafungwa Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani ... 67
6.3 Wafungwa Vijana Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani ... 69
6.4 Wafungwa Walionufaika na Msamaha na Aina ya Makosa ... 70
SURA YA SABA ... 72
UHUSIANO KATI YA UHALIFU NA VIGEZO VYA KIJAMII NA KIUCHUMI ... 72
7.0 Utangulizi ... 72
7.1 Uhusiano wa Uhalifu na Masuala ya Kijamii na Kiuchumi ... 72
7.2 Uhusiano wa Makosa ya Jinai na Idadi ya Watu, Eneo la Ardhi na Jeshi la Polisi ... 72
7.2.1 Uwiano wa Askari na Idadi ya Watu ... 72
7.2.2 Uwiano wa Askari na Ukubwa wa Eneo. ... 74
7.2.3 Idadi ya Makosa ya Jinai kwa Askari ... 74
7.3 Makosa ya Usalama Barabarani ... 74
SURA YA NANE ... 76

8.0 Utangulizi ..... 76
8.1 Nguvu Kazi ya Jeshi la Polisi, Tanzania ..... 76
SURA YA TISA ..... 79
MKAKATI WA KUKABILIANA NA UHALIFU ..... 79
9.0 Utangulizi ..... 79
9.1 Makosa Dhidi ya Binadamu ..... 80
9.2 Makosa ya Kuwania Mali ..... 81
9.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii ..... 82
9.4 Makosa ya Uhalifu wa Kifedha ..... 83
9.5 Makosa kwa Njia ya Mtandao ..... 84
9.6 Matukio ya Ajali za Barabarani ..... 85
10.0 Utangulizi ..... 86
10.1 Matukio ya Kushtua Yaliyotokea Januari - Desemba, 2019 ..... 86
11.0 Utangulizi ..... 91
11.1 Hitimisho ..... 91
11.2 Mapendekezo ..... 91

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 2.1: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania, Januari - Desemba, 2019 na 2020 ................ 5
Jedwali Na. 2.2: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020........ 6
Jedwali Na. 2.3: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 7
Jedwali Na. 2.4: Idadi ya Makosa Dhidi ya Binadamu Tanzania Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 8
Jedwali Na. 2.5: Idadi ya Makosa ya Kuwania Mali, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 9
Jedwali Na. 2.6: Makosa ya Uhalifu wa Kifedha, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ...... 9
Jedwali Na. 2.7: Idadi ya Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 10
Jedwali Na. 2.8: Idadi ya Makosa Dhidi ya Binadamu kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Januari - Desemba, 2020 ........ 11
Jedwali Na. 2.9: Idadi ya Makosa ya Kuwania Mali kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ........ 12
Jedwali Na. 2.10: Idadi ya Makosa ya Uhalifu wa Kifedha kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020........ 13
Jedwali Na. 2.11: Idadi ya Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020........ 15
Jedwali Na. 2.12: Idadi ya Makosa Madogo ya Jinai kwa Mikoa ya Kipolisi/Vikosi na Aina ya Kosa, Tanzania, Januari – Desemba, 2020........ 17
Jedwali Na. 2.13: Mauaji - Idadi ya Makosa, Watuhumiwa na Waliouawa na Sababu za Kuuawa kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ........ 19
Jedwali Na. 2.14: Migogoro ya Ardhi - Idadi ya Migogoro, Watuhumiwa, Waliouawa na Waliojeruhiwa kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ...... 20
Jedwali Na. 2.15: Idadi ya Watu Walionyanyaswa Kutokana na Makosa ya Ukatili wa Kijinsia kwa Aina ya Kosa na Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020.... 22
Jedwali Na. 2.16: Makosa ya Ukatili wa Kijinsia kwa Watoto kwa Aina ya Kosa na Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ........ 25
Jedwali Na. 2.17: Idadi ya Watu Wazima Walionyanyaswa Kutokana na Makosa ya Ukatili wa Kijinsia kwa Aina ya Kosa na Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ........ 28
Jedwali Na. 2.18: Idadi ya Kesi pamoja na Silaha na Risasi Zilizopatikana Kimkoa, Tanzania, Januari – Desemba, 2020........ 31
Jedwali Na. 2.19: Matukio ya Uhalifu Yaliyofanywa na Raia wa Kigeni kwa Aina ya Kosa na Nchi Walizotoka, Tanzania, Januari – Desemba, 2020........ 32
Jedwali Na. 2.20: Matukio Waliotendewa Raia wa Kigeni kwa Aina ya Tukio, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ........ 33
Jedwali Na. 2.21: Idadi ya Kesi na Wahamiaji Haramu kwa Jinsi, Utaifa na Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020........ 35
Jedwali Na. 2.22: Idadi ya Matukio ya Uhalifu kwa Njia ya Mtandao kwa Aina ya Tukio, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 36

Jedwali Na. 2.23: Dawa za Kulevya za Viwandani; Idadi ya Kesi na Watuhumiwa na Kiasi cha Dawa Kilichokamatwa kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ..... 37

Jedwali Na. 2.24: Dawa za Kulevya za Mashambani; Idadi ya Kesi na Watuhumiwa na Kiasi cha Dawa Kilichokamatwa kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ..... 38

Jedwali Na. 2.25: Uteketezaji wa Mashamba ya Bhangi, kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ..... 39

Jedwali Na. 2.26: Idadi ya Watu Waliouawa Kutokana na Kujichukulia Sheria Mkononi kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari hadi Desemba, 2010 hadi 2020 ..... 40

Jedwali Na. 2.27: Matukio Ya Shule Kuungua Moto kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari hadi Desemba, 2020 ..... 41

Jedwali Na. 2.28: Kesi Za Uhalifu Kabla Ya Kampeni, Wakati Wa Kampeni, Wakati Wa Kupiga Kura Na Baada Ya Matokeo Kwa Mwaka 2020 ..... 43

Jedwali Na. 2.29: Idadi ya Kesi na Jinsi Zilivyoshughulikiwa kwa Mkoa wa Kipolisi, Tanzania, Januari hadi Desemba, 2020 ..... 46

Jedwali Na. 3.1: Idadi ya Matukio ya Usalama Barabarani kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari hadi Desemba, 2020 ..... 49

Jedwali Na. 3.2: Idadi ya Ajali, Vifo, Majeruhi, Tanzania, Januari hadi Desemba, 2019 na 2020 ..... 50

Jedwali Na. 3.3: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ..... 51

Jedwali Na. 3.4: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ..... 51

Jedwali Na. 3.5: Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ..... 52

Jedwali Na. 3.6: Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ..... 53

Jedwali Na. 3.7: Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ..... 53

Jedwali Na. 3.8: Idadi ya Matukio na Waathirika katika Usafiri wa Pikipiki kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ..... 54

Jedwali Na. 3.9: Idadi ya Ajali kwa Vyanzo Vyake, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2020 ..... 55

Jedwali Na. 4.1: Idadi ya Makosa Makubwa na Madogo ya Jinai, Ajali Zilizosababisha Vifo, Vifo na Majeruhi, Tanzania, 2010- 2020 ..... 58

Jedwali Na. 5.1: Majalada Yaliyopokelewa na Kushughulikiwa kutoka Vyombo Chunguzi, Tanzania, 2020 ..... 62

Jedwali Na. 5.2: Kesi zilizoendeshwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi, Tanzania, 2020 ..... 62

Jedwali Na. 5.3: Kesi zilizoendeshwa Mahakama Kuu ..... 63

Jedwali Na. 5.4: Idadi ya Kesi zilizofunguliwa na kuisha katika Mahakama Kuu –Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ..... 63

Jedwali Na. 5.5: Jinsi kesi Zilivyokwisha katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ..... 64

Jedwali Na. 5.6: Kesi zilivyokamilika Mahakama Kuu ..... 65

Jedwali Na. 6.1: Idadi ya Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Umri, Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2020 ........ 67
Jedwali Na. 6.2: Idadi ya Wafungwa Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2020 ........ 68
Jedwali Na. 6.3: Idadi ya Wafungwa Vijana Waliopokolewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2020 ........ 69
Jedwali Na. 6.4: Idadi ya Wafungwa Walioachiwa Huru kwa Aina ya Kosa na Mkoa , Tanzania Bara, 2020 ........ 71
Jedwali Na. 7.1: Uwiano Kati ya Idadi ya Watu na Askari, Makosa ya Jinai kwa kila Askari na Idadi ya Askari kwa Kila Kilomita 100 za Mraba Kimkoa, Tanzania, Januari - Desemba, 2020 ........ 73
Jedwali Na. 7.2: Uwiano Kati ya Matukio ya Usalama Barabarani na Idadi ya Watu kwa Askari kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari - Desemba, 2020 ........ 75
Jedwali Na. 8.1: Idadi ya Maafisa, Wakaguzi na Askari Walioacha Jeshi kwa Sababu Mbalimbali, Tanzania, Januari – Desemba, 2020 ........ 76
Jedwali Na. 8.2: Nguvu Kazi na Mwelekeo wa Uwiano wa Askari kwa Idadi ya Watu, Tanzania, Januari – Desemba, 2011 - 2020 ........ 77
Jedwali Na. 8.3: Idadi ya Askari Waliojeruhiwa na Waliokufa Wakiwa Kazini kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 78
Jedwali Na. 9.1: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa Dhidi ya Binadamu, Tanzania, 2020 ........ 80
Jedwali Na. 9.2: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa ya Kuwania Mali, Tanzania, 2020 ........ 81
Jedwali Na. 9.3: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii, Tanzania, 2020. ........ 82
Jedwali Na. 9.4: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa ya Utakatishaji Fedha, Tanzania, 2020 ........ 83
Jedwali Na. 9.5: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa kwa Njia ya Mtandao, Tanzania, 2020 ........ 84
Jedwali Na. 9.6: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa ya Ajali za Barabarani, Tanzania, 2020 ........ 85

## Orodha ya Michoro

Mchoro Na. 1: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ................ 6
Mchoro Na. 2: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020........ 7
Mchoro Na. 3: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 8
Mchoro Na. 4: Ushughulikiaji wa Kesi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020............................... 47
Mchoro Na. 5: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari hadi Desemba 2019 na 2020 ........ 50
Mchoro Na. 6: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 51
Mchoro Na. 7: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 52
Mchoro Na. 8: Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020 ........ 53
Mchoro Na. 9: Vyanzo vya Ajali za Barabarani, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2020 ........ 56
Mchoro Na. 10a: Makosa Makubwa ya Jinai kwa Aina, Tanzania, Januari – Desemba, 2010 – 2020 ........ 59
Mchoro Na. 10b: Makosa Makubwa na Madogo ya Jinai, Tanzania, Januari – Desemba, 2010 – 2020 ........ 59
Mchoro Na. 10c: Makosa ya Usalama Barabarani Makubwa na Madogo, Tanzania, 2010 – 2020. 60
Mchoro Na. 10d: Matukio ya Ajali za Barabarani, Tanzania, 2010 – 2020 ..................................... 60

## DIBAJI

Wajibu wa Jeshi la Polisi Tanzania ni kuhakikisha kuwa amani inatawala, ulinzi wa raia na mali zao unaimarika, kunakuwepo na utulivu nchini ili kuwawezesha raia kufanya shughuli zao za kiuchumi bila wasi wasi wowote. Matokeo yake ni kukua kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na hatimaye Taifa.




Simoni Nyakoro Sirro
Inspekta Jenerali wa Polisi,
Jeshi la Polisi Tanzania

Mapambano dhidi ya uhalifu ni jukumu la pamoja kati ya Jeshi la Polisi, raia na wadau wengine ili kuweza kuushinda uhalifu wa aina zote. Kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia, wahalifu wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali za uhalifu na kusababisha kuibuka kwa aina mpya ya uhalifu kama makosa kwa njia ya mtandao, ugaidi, na kadhalika.

Ni dhahiri, kuwa uwezo wa Jeshi la Polisi wa kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu unakwamishwa na sababu mbalimbali zilizo nje ya Jeshi la Polisi. Sababu hizo ni pamoja na kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu ikilinganishwa na idadi ya askari waliopo nchini, upungufu wa vifaa na rasilimali fedha. Kwa kuwa ulinzi ni jukumu la kila raia, hata kama uwiano wa askari Polisi na idadi ya watu wanaohudumiwa ungefikiwa kwa kuzingatia vigezo vya kitaifa na kimataifa, bado pangekuwepo haja ya kuhamasisha na kushirikisha wadau mbalimbali wa ulinzi na usalama ili kufanikisha juhudi za Jeshi la Polisi.

Kwa kulitambua hilo, ni wito wangu kwa kila raia wa Tanzania kushiriki katika majukumu ya ulinzi na usalama wake na jirani yake pamoja na mali zao, zikiwemo mali za umma. Kila mmoja apige vita aina yoyote ya uhalifu ili kuendelea kufanya Taifa zima kuwa salama. Nitoe wito kwa kila mwanajamii kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha uhalifu hautendeki na kama ukitendeka ahakikishe kuwa mhalifu anafikishwa mbele ya vyombo vya dola ili hatua stahiki za kisheria zichukuliwe. Ni wito wangu pia kila raia atii sheria bila shuruti ili kutolazimisha Jeshi la Polisi kumlazimisha mtu kutii sheria za nchi katika kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu.



Simoni Nyakoro Sirro,
Inspekta Jenerali wa Polisi,
Makao Makuu ya Polisi.
S.L.P. 961,
Dodoma,
Tanzania.

INSPEKTA JENERALI WA POLISI

## SHUKURANI

Taarifa hii imeandaliwa kwa pamoja na wadau mbalimbali wakiongozwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini Tanzania, Simon Nyakoro Sirro (IGP). Namshukuru kwa kutoa maelekezo na kututia moyo wakati wa uandaaji wa taarifa hii. Vilevile shukrani zangu ziende kwa wasaidizi wote kwa jitihada zao zilizosaidia uandaaji na uchapishaji wa taarifa hii.



Robert Boaz - CP
Mkurungezi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai,
Jeshi la Polisi Tanzania

Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Dk. Albina Chuwa, Kamishna Jenerali wa Magereza Major Gen. Suleiman Mungiya Mzee na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Ndugu. Biswalo E. K. Mganga kwa kuwaruhusu watendaji wao kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuandaa taarifa.

Shukrani pia ziwafikie Maafisa, Wakaguzi, na Askari wa vyeo mbalimbali wote nchini kwa mchango wao walioutoa kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha uandaaji wa taarifa hii na kwa namna ya pekee nitoe shukrani kwa wajumbe wa kamati ya uandaaji wa taarifa hii kutoka Jeshi la Polisi nchini, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Jeshi la Magereza na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini. Kamati hii inahusisha wajumbe 20 wakiongozwa na SACP. Andrew Jumamosi (TPF), Tumaini Kweka, Mkurugenzi Msaidizi- Usimamizi wa Kesi (NPS), Sikujua Emmauel (TPS), ASP Fatuma Mandai (TPF), INSP Hamad Manugwa (TPF), A/INSP Juma Hebu (TPF), WP.3071 D/SGT Sophia Ninje (TPF), D.8672 D/SGT Praygod Mbwambo (TPF), WP.5246 D/CPL Habiba Maganga (TPF), G.1254 D/C Vitalis Wantiku (TPF), G.3258 D/C John Nyemba (TPF), G.8396 D/C Baraka Kachira (TPF), H. 3324 D/C Hamisi Mlambo (TPF), H.3712 D/C Elia Kuguru (TPF), H.3769 D/C Mohamed Athumani (TPF), H.3384 D/C Jidula Mabomba (TPF), H.8686 D/C Fredrick Rubaba (TPF), Hawa Mfangavo (TPF), Trilas Mwanry (TPF), Valerian Tesha (NBS) na Margreth Jacob (NBS).

Robert Boaz – CP,
Mkurungenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai,
Makao Makuu ya Upelelezi,
S.L.P. 52,
Dodoma,
Tanzania.

MKURUGENZI WA
UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI

# MAANA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| A/INSP | - | Mkaguzi Msaidizi wa Polisi |
| ASP | - | Mrakibu Msaidizi wa Polisi |
| ATM | - | Mashine zinazotumika kutoa/kuweka fedha benki |
| CP-CP | - | Kamishna wa Polisi Jamii |
| D/C | - | Mpelelezi wa Cheo cha Konstebo |
| D/CPL | - | Mpelelezi wa Cheo cha Koplo |
| D/SGT | - | Mpelelezi wa Cheo cha Sajenti |
| DCI | - | Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai |
| IGP | - | Inspekta Jenerali wa Polisi |
| INSP | - | Mkaguzi wa Polisi/Magereza |
| NBS | - | Ofisi ya Taifa ya Takwimu |
| NFA | - | Hakuna hatua iliyochukuliwa |
| NOD | - | Hakuna kosa lililobainika |
| OC CID | - | Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya |
| NPS | - | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka |
| NPSA | | Sheria ya Huduma ya Taifa ya Mashtaka |
| PSV | - | Magari yaliyoruhusiwa na Serikali kubeba abiria |
| RPC | - | Kamanda wa Polisi wa Mkoa |
| SACP | - | Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi |
| SAR | - | Silaha Ndogo ya Kivita |
| SMG | - | Silaha ya Kivita |
| SP | - | Mrakibu wa Polisi |
| SSA | - | Wakili wa Serikali Mwandamizi |
| SSP | - | Mrakibu Mwandamizi wa Polisi |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TPF | - | Jeshi la Polisi Tanzania |
| TPS | - | Jeshi la Magereza Tanzania |
| TZS | - | Shilingi ya Tanzania |
| “U” | - | Hakuna mtuhumiwa aliyekamatwa |
| UNHCR | - | Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi |
| UN-ISCCJ | - | Taarifa ya Umoja wa Mataifa ya Takwimu ya Haki za Wahalifu na Uhalifu |

# MUHTASARI

Taarifa ya hali ya uhalifu ya kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 imeangalia kwa ujumla matukio mbalimbali ya uhalifu yaliyoripotiwa katika vituo vya Polisi nchini katika kipindi hicho. Matukio yamegawanywa katika makundi mawili ambayo ni makosa makubwa na madogo ya jinai na ya Usalama barabarani. Makosa ya jinai yamegawanywa katika makundi matatu; makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020, jumla ya matukio 2,737,711 ya jinai na Usalama barabarani yaliripotiwa katika vituo vya Polisi nchini yakilinganishwa na jumla ya matukio 2,907,333 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 169,622 sawa na asilimia 5.8.

Kwa upande wa matukio ya jinai, kumekuwa na upungufu wa makosa 9,626 sawa na asilimia 1.6 kutoka matukio 583,245 yaliyoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020, ukilinganisha na matukio 592,871 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka, 2019. Katika matukio yote ya jinai yaliyoripotiwa kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020, matukio makubwa yalikuwa 50,689 na madogo 532,556 ambapo kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2019 matukio makubwa yalikuwa 58,590 na madogo 534,281 na hivyo kuwa na upungufu wa makosa makubwa 7,901 sawa na asilimia 13.5 na upungufu wa makosa madogo 1,725 sawa na asilimia 0.3.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 matukio ya Usalama barabarani yaliyoripotiwa yalikuwa 2,154,466 yakilinganishwa na matukio 2,314,462 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 159,996 sawa na asilimia 6.9. Katika matukio yote ya Usalama barabarani, matukio makubwa (ajali) yalikuwa 1,933 na matukio madogo (tozo) yalikuwa 2,152,533 yakilinganishwa na matukio makubwa 2,924 na matukio madogo 2,311,538 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2019, huu ni upungufu wa matukio makubwa 991, sawa na asilimia 33.9 na upungufu wa matukio madogo 159,005, sawa na asilimia 6.9.

Aidha katika matukio ya ajali yaliyoripotiwa kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 watu 1,384 walipoteza maisha na watu 2,362 walijeruhiwa wakilinganishwa na watu 1,536 waliopoteza maisha na watu 3,123 walijeruhiwa kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2019 ikiwa ni upungufu wa vifo 177 (asilimia 14.7) na majeruhi 761 (asilimia 24.4). Pia matukio ya ajali za pikipiki nchini katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 yalikuwa jumla ya matukio 505 yaliripotiwa ikilinganishwa na matukio 628 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 123 sawa na asilimia 19.6.

Vilevile, jamii iliendelea kushuhudia vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vile kubaka, kulawiti, kutupa watoto, wizi wa watoto, na ukeketaji. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya watu 42,414 walifanyiwa ukatili wa kijinsia ikilinganishwa na watu 39,365 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2019. Hili ni ongezeko la watu 3,049 sawa na asilimia 7.7.

# SURA YA KWANZA

## USULI

### 1.0 Utangulizi

Sura hii inaangalia jiografia ya nchi na majukumu ya msingi ya Jeshi la Polisi Tanzania. Takwimu za hali ya uhalifu nchini zinalisaidia Jeshi la Polisi katika kupanga mipango na programu za muda mfupi, kati na mrefu ili kudhibiti hali ya uhalifu nchini na kuendeleza hali ya amani na utulivu iliyopo ambayo ni muhimu katika kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii kufikia malengo ya uchumi wa viwanda.

### 1.1 Jiografia na Utawala

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muungano wa nchi mbili huru za Tanganyika na Zanzibar ulioundwa tarehe 26 Aprili 1964. Tanzania ipo kati ya latitudo $1^0$ na $12^0$ kusini mwa Ikweta; na kati ya longitudo 290 na 410 mashariki mwa Greenwich. Tanzania ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 945,087. Kwa upande wa kaskazini imepakana na nchi za Kenya na Uganda; kwa upande wa magharibi imepakana na nchi za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; kwa upande wa kusini magharibi imepakana na nchi za Malawi na Zambia; kwa upande wa kusini imepakana na nchi ya Msumbiji; na kwa upande wa mashariki imepakana na Bahari ya Hindi.

Tanzania ina maziwa makuu matatu ambayo ni Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Tanzania ina vivutio vingi vya kitalii ukiwemo mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote Afrika na wenye theluji kwa kipindi chote cha mwaka. Vivutio vingine ni pamoja na mbuga za wanyama, mambo ya kale na fukwe nzuri za bahari katika Pwani ya Tanzania Bara na visiwa vya Tanzania Zanzibar, yaani Unguja na Pemba.

Hali ya hewa ni ya kitropiki yenye misimu miwili ya mvua ya masika na vuli katika sehemu kubwa ya nchi. Shughuli kuu za uchumi ni kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji madini, utalii, viwanda na huduma. Kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Makadirio ya idadi ya watu kwa mwaka 2020 ni watu 57,637,628. Licha ya kuwa Tanzania ina makabila yanayozidi 120, lugha kuu ya Taifa ni Kiswahili kinachozungumzwa takribani na watu wote.

Tanzania ni nchi inayofuata demokrasia ya vyama vingi. Dola ya Tanzania ina mihimili mitatu - Bunge, Mahakama na Serikali yenye mfumo wa serikali mbili - Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshaongozwa na Marais watano na ile ya Zanzibar imeshaongozwa na Marais nane.

Kiutawala, Tanzania imegawanyika katika mikoa 31 ambapo 26 ipo Tanzania Bara na mitano (5) ipo Tanzania Zanzibar.

### 1.2 Jeshi la Polisi Tanzania

Jeshi la Polisi limeanzishwa kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 kama ilivyoboreshwa mwaka 2002. Pamoja na kuzingatia sheria na katiba ya nchi, pia Jeshi la Polisi huongozwa kwa kuzingatia kanuni za kudumu za Jeshi "Police General Orders" zenye misingi (vithaminiwa) ya ujasiri, uwazi, utiifu, ukweli, uadilifu, uaminifu, haki na kuheshimiana. Aidha, katika kutekeleza majukumu yake, Jeshi la Polisi huzingatia mikataba ya kimataifa ya kiusalama na haki za binadamu.

Muundo wa Jeshi la Polisi umegawanyika katika Kamisheni nane (8) za kiutendaji, ambazo ni Kamisheni ya Utawala na Menejimenti ya Rasilimali watu, Kamisheni ya Fedha na Lojistiki, Kamisheni ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Kamisheni ya Operesheni na Mafunzo, Kamisheni ya Ushirikishwaji wa Jamii, Kamisheni ya Zanzibar, Kamisheni ya Intelijensia na Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi.

Kiutawala, Jeshi la Polisi lina mikoa 35, ambapo mikoa 30 iko Tanzania Bara na mikoa 5 iko Tanzania Zanzibar na vikosi 12.

#### 1.2.1 Majukumu ya Jeshi la Polisi

Majukumu ya Jeshi la Polisi yameainishwa katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 kama ilivyoboreshwa mwaka 2002. Majukumu hayo ni pamoja na kulinda amani; kulinda raia na mali zao; kuzuia makosa kabla hayajatendeka; kuwakamata wahalifu na kuwafikisha mahakamani na kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za nchi.

#### 1.2.2 Takwimu za Jeshi la Polisi

Jeshi la Polisi lina Takwimu za aina mbili - Takwimu za kiutawala na za uhalifu. Takwimu za kiutawala zinajumuisha rasilimali watu, vifaa na fedha. Takwimu za uhalifu zinajumuisha makosa ya jinai na matukio ya Usalama barabarani yanayoripotiwa katika vituo vya Polisi nchini. Takwimu hizi huliwezesha Jeshi la Polisi kupanga mipango yake ya kiutendaji na kubuni mbinu mbalimbali za kupambana na uhalifu nchini.

### 1.2.3 Kitengo cha Takwimu cha Jeshi la Polisi

Kitengo cha takwimu cha Jeshi la Polisi kinajukumu la kupokea taarifa zote za uhalifu zinazoripotiwa katika vituo vya Polisi nchini na kuzifanyia kazi kwa kuzichambua na kuzihifadhi na hatimaye kuandaa taarifa ya hali ya uhalifu nchini kwa kila robo, nusu na ya mwaka. Baada ya kukamilisha uandaaji wa taarifa hizo, husambazwa ndani ya Jeshi la Polisi na wadau wengine.

Kitengo cha Takwimu kina mfumo wa kielektroniki uitwao Crime Statistics Management Information System (CSMIS) unaowezesha kupokea taarifa za uhalifu kutoka katika mikoa yote nchini. Mfumo huu umeanza kufanya kazi katika vituo vikuu 20 kwa Kanda ya Dar es Salaam na ofisi za Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa (RCOs) ambapo baadaye kuendelezwa hadi kufikia ngazi ya vituo vyote vya Polisi nchini.

Lengo kuu la mfumo huu wa kielektroniki ni kurahisisha upokeaji na utunzaji wa taarifa zote za uhalifu na utawala ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kuchambua na kutoa taarifa bora na kwa wakati.

# SURA YA PILI

## HALI YA UHALIFU NCHINI

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inaonesha kwa ujumla matukio mbalimbali ya uhalifu yaliyoripotiwa nchini kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020. Matukio hayo yamegawanywa katika sehemu kuu mbili ambazo ni Makosa ya Jinai na ya Usalama Barabarani. Aidha, sehemu hizo zimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni makosa makubwa na madogo.

a. Makosa ya Jinai

i. *Makosa makubwa ya jinai;* ni yale ambayo yamepewa kipaumbele na Jeshi la Polisi katika kuyashughulikia na mengi ya makosa haya yana madhara makubwa ambayo huonekana moja kwa moja katika jamii. Kwa mfano mauaji, unyang'anyi wa aina zote na kupatikana na madawa ya kulevya.

ii. *Makosa madogo ya jinai;* ni yale ambayo yanapotendeka hayana madhara makubwa katika jamii kwa mfano wizi kutoka maungoni, shambulio la kawaida, na lugha ya matusi.

b. Makosa ya Usalama Barabarani

i. *Makosa makubwa ya usalama barabarani;* ni matukio ya ajali za barabarani yanayosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali.

ii. *Makosa madogo ya usalama barabarani:* ni makosa ambayo yakifanyika hayaleti madhara kwa wakati huo kama vile kuendesha vyombo vya moto bila leseni ya udereva na vibali vingine, kuegesha chombo bila kufuata utaratibu, kwenda mwendo kasi, kupita njia au barabara isiyoruhusiwa, kuendesha gari bovu nakutokufunga mkanda. Pamoja na makosa hayo kutokuleta madhara kwa wakati huo, makosa hayo huweza kuwa vyanzo vya ajali kama hayakuzingatiwa. Mkosaji anapokamatwa hupewa adhabu ya kifungo, kutozwa faini au hupewa onyo.

### 2.1 Takwimu za Uhalifu Tanzania

Sehemu hii inaonesha majedwali na michoro ya hali ya uhalifu nchini kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2019. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020, jumla ya matukio 2,737,711 ya jinai na usalama barabarani yaliripotiwa katika vituo vya Polisi nchini, ikilinganishwa na matukio 2,907,333 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 169,622 sawa na asilimia 5.8.

Takwimu zinaonesha jumla ya matukio makubwa na madogo ya jinai 583,245 yaliyoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 ikilinganishwa na matukio 592,871 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka, 2019. Huu ni upungufu wa matukio 9,626 sawa na asilimia 1.6.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020, matukio makubwa ya jinai yalikuwa 50,689 ikilinganishwa na matukio 58,590 kipindi kama hicho cha mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 7,901 sawa na asilimia 13.5.

Matukio madogo ya jinai yalikuwa 532,556 katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 ikilinganishwa na matukio 534,281 kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 1,725 sawa na asilimia 0.3.

Jumla ya matukio makubwa na madogo ya Usalama barabarani yalikuwa 2,154,466 katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020, ikilinganishwa na matukio 2,314,462 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 159,996 sawa na asilimia 6.9.

Matukio makubwa ya usalama barabarani yalikuwa 1,933 katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 ikilinganishwa na matukio 2,924 kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 991 sawa na asilimia 33.9.

Matukio madogo ya usalama barabarani yalikuwa 2,152,533 katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 ikilinganishwa na matukio 2,311,538 kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 159,005 sawa na asilimia 6.9.


Katika kudhibiti makosa ya usalama barabarani, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 Jeshi la Polisi lilikusanya jumla ya TZS 64,967,023,850 ikiwa ni tozo ya makosa mbalimbali ikilinganishwa na TZS 69,153,184,500 zilizokusanywa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2019. Huu ni upungufu wa TZS 4,186,760,650 ambao ni sawa na upungufu wa asilimia 6.1 ya fedha za tozo za makosa ya usalama barabarani zilizokusanywa mwaka 2020.

**Jedwali Na. 2.1: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania, Januari - Desemba, 2019 na 2020**

| Aina ya Kosa | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| **Jinai** | | | | |
| Madogo | 534,281 | 532,556 | -1,725 | -0.3 |
| Makubwa | 58,590 | 50,689 | -7,901 | -13.5 |
| **Jumla Ndogo** | **592,871** | **583,245** | **-9,626** | **-1.6** |
| **Usalama Barabarani** | | | | |
| Madogo | 2,311,538 | 2,152,533 | -159,005 | -6.9 |
| Makubwa | 2,924 | 1,933 | -991 | -33.9 |
| **Jumla Ndogo** | **2,314,462** | **2,154,466** | **-159,996** | **-6.9** |
| **Jumla Kuu** | **2,907,333** | **2,737,711** | **-169,622** | **-5.8** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

**Mchoro Na. 1: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020**





Jedwali Na.2.2 na Mchoro Na.2 yanaonesha mchanganuo wa makosa ya jinai na matukio ya usalama barabarani Tanzania Bara kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2019 na 2020.

**Jedwali Na. 2.2: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Aina ya Kosa | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| **Jinai** | | | | |
| Madogo | 530,525 | 526,941 | -3,584 | -0.7 |
| Makubwa | 55,730 | 47,712 | -8,018 | -14.4 |
| **Jumla Ndogo** | **586,255** | **574,653** | **-11,602** | **-2.0** |
| | | | | |
| **Usalama Barabarani** | | | | |
| Madogo | 2,292,647 | 2,137,251 | -155,396 | -6.8 |
| Makubwa | 2,704 | 1,714 | -990 | -36.6 |
| **Jumla Ndogo** | **2,295,351** | **2,138,965** | **-156,386** | **-6.8** |
| | | | | |
| **Jumla Kuu** | **2,881,606** | **2,713,618** | **-167,988** | **-5.8** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

**Mchoro Na. 2: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020**





Jedwali Na.2.3 na Mchoro Na.3 yanaonesha mchanganuo wa makosa ya jinai na matukio ya usalama barabarani Tanzania Zanzibar kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2019 na 2020.

**Jedwali Na. 2.3: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| **Aina ya Kosa** | **2019** | **2020** | **Tofauti** | **Badiliko (asilimia)** |
|---|---|---|---|---|
| **Jinai** | | | | |
| Madogo | 3,756 | 5,615 | 1,859 | 49.5 |
| Makubwa | 2,860 | 2,977 | 117 | 4.1 |
| **Jumla Ndogo** | **6,616** | 8,592 | 1,976 | 29.9 |
| **Usalama Barabarani** | | | | |
| Madogo | 18,891 | 15,282 | -3,609 | -19.1 |
| Makubwa | 220 | 219 | -1 | -0.5 |
| **Jumla Ndogo** | **19,111** | 15,501 | -3,610 | -18.9 |
| **Jumla Kuu** | **25,727** | 24,093 | -1,634 | -6.4 |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

**Mchoro Na. 3: Idadi na Aina ya Makosa, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020**




## 2.2 Uchambuzi wa Makosa Makubwa ya Jinai

Makosa makubwa ya jinai ni pamoja na makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii. Uchambuzi umefanyika kwa kuelezea aina ya makosa yaliyoripotiwa katika kila kundi.

### 2.2.1 Makosa Dhidi ya Binadamu

Kundi hili linahusisha makosa ya mauaji, kubaka, kulawiti, wizi wa watoto, kutupa watoto, kunajisi na usafirishaji haramu wa binadamu. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya makosa 11,001 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 12,223 kwa mwaka 2019. Huu ni upungufu wa makosa 1,222 sawa na asilimia 10.0. Makosa yenye ongezeko kubwa la idadi ni Kunajisi (23), Kutupa watoto (5) na Usafirishaji haramu binadamu (1). Aidha, makosa yaliyopungua sana kiidadi ni Kubaka (574), Mauaji (394) na Kulawiti (278) (Jedwali Na. 2.4).

**Jedwali Na. 2.4: Idadi ya Makosa Dhidi ya Binadamu Tanzania Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Kosa | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Mauaji | 2,619 | 2,225 | -394 | -15.0 |
| Kubaka | 7,837 | 7,263 | -574 | -7.3 |
| Kulawiti | 1,483 | 1,205 | -278 | -18.7 |
| Wizi wa Watoto | 89 | 84 | -5 | -5.6 |
| Kutupa Watoto | 148 | 153 | 5 | 3.4 |
| Kunajisi | 29 | 52 | 23 | 79.3 |
| Usafirishaji Haramu wa Binadamu | 18 | 19 | 1 | 5.6 |
| **Jumla** | **12,223** | **11,001** | **-1,222** | **-10.0** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

### 2.2.2 Makosa ya Kuwania Mali

Kundi hili linahusisha makosa ya unyang'anyi, uvunjaji, wizi, kuchoma nyumba moto na uhalifu wa kifedha. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya makosa 24,961 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 28,853 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa makosa 3,892 sawa na asilimia 13.5 (Jedwali Na. 2.5).

**Jedwali Na. 2.5: Idadi ya Makosa ya Kuwania Mali, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Kosa | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Wizi wa Silaha | 15 | 17 | 2 | 13.3. |
| Unyang'anyi katika Barabara Kuu | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Unyang'anyi wa Kutumia Silaha | 405 | 297 | -108 | -26.7 |
| Unyang'anyi wa Kutumia Nguvu | 2,122 | 1,482 | -640 | -30.2 |
| Uvunjaji | 14,809 | 12,486 | -2,323 | -15.7 |
| Wizi | 126 | 87 | -39 | -31.0 |
| Wizi wa Pikipiki | 4,902 | 4,823 | -79 | -1.6 |
| Wizi wa Magari | 184 | 175 | -9 | -4.9 |
| Wizi wa Mifugo | 4,097 | 3,707 | -390 | -9.5 |
| Kuchoma Nyumba Moto | 975 | 982 | 7 | 0.7 |
| Uhalifu wa Kifedha | 1,218 | 905 | -313 | -25.7 |
| **Jumla** | **28,853** | **24,961** | **-3,895** | **-13.5** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

### Makosa ya Uhalifu wa Kifedha

Makosa haya ni mwendelezo wa makosa yaliyo katika kundi la kuwania mali, ambayo ni kughushi, noti bandia, wizi katika mabenki, mashirika ya umma, Serikali kuu/mitaa na vyama vya siasa. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya makosa 905 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 1,218 yaliripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa makosa 313 sawa na asilimia 25.7. (Jedwali Na.2.6).

**Jedwali Na. 2.6: Makosa ya Uhalifu wa Kifedha, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Makosa | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Noti Bandia | 293 | 78 | -215 | -73.4 |
| Wizi katika Mabenki | 1 | 0 | -1 | -100.0 |
| Wizi katika Mashirika ya Umma | 87 | 50 | -37 | -42.5 |
| Wizi katika Vyama vya Ushirika | 11 | 4 | -7 | -63.6 |
| Wizi katika Serikali za Mitaa | 21 | 6 | -15 | -71.4 |
| Wizi katika Serikali Kuu | 24 | 23 | -1 | -4.2 |
| Wizi katika Vyama vya Siasa | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Kughushi | 781 | 744 | -37 | -4.7 |
| **Jumla** | **1,218** | **905** | **-313** | **-25.7** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

### 2.2.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii

Kundi hili linahusisha makosa ya kupatikana na dawa za kulevya, nyara za Serikali, silaha, risasi, pombe ya moshi, mazao ya misitu, rushwa, magendo na wahamiaji haramu. Jumla ya makosa 14,727 yaliripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 ikilinganishwa na makosa 17,514 kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa makosa 2,787 sawa na asilimia 15.9. Makosa yaliyochangia upungufu huo ni kupatikana na; pombe ya moshi (1,009); bangi (580), magendo (352) na nyara za serikali (286). Mafanikio katika kudhibiti makosa yaliyomo katika kundi hili kwa sehemu kubwa yanatokana na juhudi za Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama pamoja na wananchi kwa ujumla. Kwa upande mwingine makosa yenye ongezeko kwa idadi ni kupatikana na; mirungi (96), risasi (17) na mazao ya bahari (4), (Jedwali Na.2.7).

**Jedwali Na. 2.7: Idadi ya Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Makosa | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Kupatikana na Silaha | 303 | 169 | -134 | -44.2 |
| Dawa za Kulevya | 502 | 429 | -73 | -14.5 |
| Bangi | 6,483 | 5903 | -580 | -8.9 |
| Mashamba ya Bangi | 31 | 27 | -4 | -12.9 |
| Mirungi | 935 | 1031 | 96 | 10.3 |
| Nyara za Serikali | 1,014 | 728 | -286 | -28.2 |
| Magendo | 684 | 332 | -352 | -51.5 |
| Rushwa | 5 | 3 | -2 | -40.0 |
| Pombe ya Moshi | 5,611 | 4,602 | -1,009 | -18.0 |
| Kupatikana na Mitambo* | 374 | 311 | -63 | -16.8 |
| Kupatikana na Risasi | 46 | 63 | 17 | 37.0 |
| Kupatikana na Bomu | 2 | 0 | -2 | -100.0 |
| Uvuvi Haramu | 145 | 23 | -122 | -84.1 |
| Kupatikana na Mazao ya Misitu | 334 | 233 | -101 | -30.2 |
| Kupatikana na Mazao ya Bahari | 7 | 11 | 4 | 57.1 |
| Wahamiaji Haramu | 1,038 | 862 | -176 | -17.0 |
| **Jumla** | **17,514** | **1,4727** | **-2,787** | **-15.9** |

**Mitambo ya pombe moshi*
Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

## 2.3 Uchambuzi wa Makosa Makubwa ya Jinai kwa Mikoa ya Kipolisi

Katika sehemu hii, makosa makubwa ya jinai yametenganishwa kimkoa kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Takwimu zinaonesha tofauti ya makosa kimkoa kutokana na kundi na idadi ya makosa yaliyoripotiwa.

### 2.3.1 Makosa Dhidi ya Binadamu

Mikoa iliyoongoza kwa makosa dhidi ya binadamu yaliyoripotiwa katika mikoa ya kipolisi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa mwaka 2020 ni Kinondoni (637) , Dodoma (608), Kilimanjaro (606), Tanga (546) na Mbeya (507). Mikoa ya kipolisi yenye idadi ndogo ya makosa ni Bandari (1), Reli (1), Singida (66), Kaskazini pemba (82) na Kusini unguja (98). Aina ya makosa yaliyoongoza kwa idadi

ya matukio ni kubaka (7,263), mauaji (2,225), kulawiti (1,205), kutupa watoto (153) na wizi wa watoto (84) (Jedwali Na.2.8).

**Jedwali Na. 2.8: Idadi ya Makosa Dhidi ya Binadamu kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Januari - Desemba, 2020**

| Mkoa | Mauaji | Kubaka | Kutupa Watoto | Kulawiti | Wizi wa Watoto | Kunajisi | Usafirishaji Binadamu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 39 | 241 | 21 | 78 | 3 | 0 | 3 | 385 |
| Ilala | 56 | 293 | 13 | 63 | 11 | 0 | 2 | 438 |
| Temeke | 26 | 214 | 4 | 93 | 6 | 0 | 0 | 343 |
| Kinondoni | 83 | 381 | 16 | 150 | 6 | 0 | 1 | 637 |
| Dodoma | 119 | 358 | 0 | 127 | 4 | 0 | 0 | 608 |
| Geita | 82 | 169 | 2 | 13 | 5 | 0 | 0 | 271 |
| Iringa | 68 | 196 | 9 | 34 | 2 | 1 | 0 | 310 |
| Kagera | 163 | 237 | 11 | 3 | 7 | 0 | 0 | 421 |
| Katavi | 56 | 91 | 1 | 7 | 2 | 0 | 0 | 157 |
| Kigoma | 111 | 287 | 12 | 43 | 3 | 0 | 0 | 456 |
| Kilimanjaro | 72 | 418 | 17 | 94 | 2 | 3 | 0 | 606 |
| Lindi | 56 | 192 | 0 | 16 | 0 | 0 | 0 | 264 |
| Mara | 74 | 203 | 0 | 18 | 0 | 0 | 0 | 295 |
| Manyara | 64 | 156 | 1 | 45 | 1 | 0 | 1 | 268 |
| Mbeya | 92 | 348 | 15 | 44 | 3 | 0 | 5 | 507 |
| Morogoro | 90 | 315 | 2 | 45 | 0 | 0 | 0 | 452 |
| Mtwara | 50 | 154 | 1 | 19 | 1 | 0 | 0 | 225 |
| Mwanza | 103 | 207 | 8 | 30 | 11 | 0 | 0 | 359 |
| Njombe | 87 | 303 | 3 | 14 | 1 | 0 | 0 | 408 |
| Pwani | 56 | 268 | 0 | 37 | 1 | 0 | 4 | 366 |
| Rufiji | 22 | 128 | 1 | 25 | 2 | 0 | 0 | 178 |
| Rukwa | 60 | 188 | 2 | 5 | 1 | 1 | 0 | 257 |
| Ruvuma | 37 | 112 | 1 | 8 | 1 | 0 | 0 | 159 |
| Shinyanga | 83 | 248 | 2 | 18 | 3 | 0 | 0 | 354 |
| Simiyu | 39 | 118 | 1 | 6 | 0 | 0 | 3 | 167 |
| Singida | 51 | 13 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 66 |
| Songwe | 68 | 116 | 1 | 9 | 1 | 1 | 0 | 196 |
| Tabora | 152 | 225 | 0 | 29 | 3 | 0 | 0 | 409 |
| Tanga | 70 | 431 | 5 | 39 | 1 | 0 | 0 | 546 |
| Tarime - Rorya | 62 | 76 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 140 |
| Wanamaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Reli | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Tazara | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Viwanja vya Ndege | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Bandari | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Tanzania Bara** | **2,192** | **6,686** | **150** | **1,115** | **82** | **6** | **19** | **10,250** |
| Kaskazini Pemba | 2 | 68 | 0 | 3 | 0 | 9 | 0 | 82 |
| Kaskazini Unguja | 5 | 87 | 0 | 5 | 1 | 7 | 0 | 105 |
| Kusini Pemba | 5 | 86 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 | 100 |
| Kusini Unguja | 8 | 77 | 1 | 10 | 0 | 2 | 0 | 98 |
| Mjini Magharibi | 13 | 259 | 1 | 65 | 1 | 28 | 0 | 368 |
| **Tanzania Zanzibar** | **33** | **577** | **3** | **90** | **2** | **46** | **0** | **753** |
| **Tanzania** | **2,225** | **7,263** | **153** | **1,205** | **84** | **52** | **19** | **11,001** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

### 2.3.2 Makosa ya Kuwania Mali

Jedwali Na. 2.9 linaonesha mgawanyo wa makosa ya kuwania mali katika mikoa ya kipolisi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa mwaka 2020. Mikoa ya kipolisi yenye idadi kubwa ya makosa ni Kinondoni (2,769), Ilala (2,363), Dodoma (1,311), Morogoro (1,207), na Kagera (1,068).

Makosa yaliyoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ni uvunjaji (12,486), wizi wa pikipiki (4,823), wizi wa mifugo (3,707), unyang'anyi wa kutumia nguvu (1,482) na kuchoma nyumba moto (982).

**Jedwali Na. 2.9: Idadi ya Makosa ya Kuwania Mali kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020**

**Jedwali Na. 3.2: Idadi ya Ajali, Vifo, Majeruhi, Tanzania, Januari hadi Desemba, 2019 na 2020**

| Tukio | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Matukio ya Ajali | 2,924 | 1,933 | -991 | -33.9 |
| Ajali zilizosababisha Vifo | 1,208 | 1,031 | -177 | -14.7 |
| Ajali zilizosababisha Majeruhi | 1,026 | 646 | -380 | -37.0 |
| Ajali za Kawaida | 690 | 256 | -434 | -62.9 |
| Watu Waliokufa | 1,536 | 1,384 | -152 | -9.9 |
| Watu Waliojeruhiwa | 3,123 | 2,362 | -761 | -24.4 |

**Mchoro Na. 5: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari hadi Desemba 2019 na 2020**




Matukio ya usalama barabarani yamechambuliwa kwa kutofautisha Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kama ilivyo katika Jedwali Na. 3.3 na 3.4 na Michoro Na. 6 na 7 ambayo yanaonesha idadi ya matukio ya ajali, ajali zilizosababisha vifo, idadi ya watu waliokufa na majeruhi waliotokana na ajali hizo.

**Jedwali Na. 3.3: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Tukio | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Matukio ya Ajali | 2,704 | 1,714 | -990 | -36.6 |
| Ajali zilizosababisha Vifo | 1,122 | 915 | -207 | -18.4 |
| Ajali zilizosababisha Majeruhi | 918 | 564 | -354 | -38.6 |
| Ajali za Kawaida | 664 | 235 | -429 | -64.6 |
| Watu Waliokufa | 1,432 | 1,260 | -172 | -12.0 |
| Watu Waliojeruhiwa | 2,833 | 2,070 | -763 | -26.9 |


**Mchoro Na. 6: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020**




**Jedwali Na. 3.4: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Tukio | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Matukio ya Ajali | 220 | 219 | -1 | -0.5 |
| Ajali zilizosababisha Vifo | 86 | 116 | 30 | 34.9 |
| Ajali zilizosababisha Majeruhi | 108 | 82 | -26 | -24.1 |
| Ajali za Kawaida | 26 | 21 | -5 | -19.2 |
| Watu Waliokufa | 104 | 124 | 20 | 19.2 |
| Watu Waliojeruhiwa | 290 | 292 | 2 | 0.7 |

**Mchoro Na. 7: Idadi ya Ajali, Vifo na Majeruhi, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020**




## 3.2 Ajali za Pikipiki

Kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 pikipiki ziliendelea kuwa chombo cha usafirishaji kilichokuwa kinatumiwa na wananchi katika shughuli mbalimbali kama njia rahisi zaidi ya usafirishaji wa abiria na mizigo mijini na vijijini. Licha ya nia njema ya Serikali ya kuwapunguzia wananchi adha ya usafiri, pikipiki zimekuwa mojawapo ya vyanzo vikubwa vya ajali za barabarani.


Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya matukio 505 ya ajali za pikipiki yaliripotiwa ikilinganishwa na matukio 628 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Huu ni upungufu wa matukio 123 sawa na asilimia 19.6 (Jedwali Na. 3.5 na Mchoro Na. 8).

**Jedwali Na. 3.5: Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Tukio | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Ajali za Pikipiki | 628 | 505 | -123 | -19.6 |
| Watu Waliokufa | 355 | 319 | -36 | -10.1 |
| Watu Waliojeruhiwa | 526 | 422 | -104 | -19.8 |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

**Mchoro Na. 8: Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020**




Jedwali Na. 3.6 na 3.7 yanaonesha matukio ya ajali za pikipiki, watu waliokufa na kujeruhiwa kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2019 na 2020.

**Jedwali Na. 3.6: Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Tukio | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Ajali za Pikipiki | 549 | 415 | -134 | -24.4 |
| Watu Waliokufa | 312 | 261 | -51 | -16.3 |
| Watu Waliojeruhiwa | 454 | 313 | -141 | -31.1 |

**Jedwali Na. 3.7: Idadi ya Ajali za Pikipiki, Vifo na Majeruhi, Tanzania Zanzibar, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| Tukio | 2019 | 2020 | Tofauti | Badiliko (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Ajali za Pikipiki | 79 | 90 | 11 | 13.9 |
| Watu Waliokufa | 43 | 58 | 15 | 34.9 |
| Watu Waliojeruhiwa | 72 | 109 | 37 | 51.4 |

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020, mikoa ya kipolisi iliyoongoza kwa kuwa na ajali nyingi za pikipiki ni Kinondoni (64), Mjini Magharibi (44), Ilala (42), Kilimanjaro (30) na Lindi (23) (Jedwali Na. 3.8).

**Jedwali Na. 3.8: Idadi ya Matukio na Waathirika katika Usafiri wa Pikipiki kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2020**

| Mkoa | Jumla ya Matukio | Matukio ya Ajali | Watu Waliokufa | | Watu Waliojeruhiwa | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | Me | Ke |
| Arusha | 17 | 12 | 6 | 0 | 12 | 0 |
| Ilala | 56 | 42 | 13 | 1 | 33 | 13 |
| Temeke | 23 | 22 | 1 | 0 | 21 | 0 |
| Kinondoni | 84 | 64 | 16 | 0 | 43 | 11 |
| Dodoma | 4 | 3 | 2 | 0 | 3 | 0 |
| Geita | 13 | 8 | 4 | 0 | 6 | 0 |
| Iringa | 11 | 5 | 8 | 0 | 4 | 0 |
| Kagera | 18 | 13 | 8 | 0 | 6 | 1 |
| Katavi | 23 | 19 | 11 | 0 | 12 | 0 |
| Kigoma | 12 | 9 | 6 | 0 | 6 | 0 |
| Kilimanjaro | 51 | 30 | 27 | 0 | 24 | 0 |
| Lindi | 30 | 23 | 17 | 1 | 13 | 0 |
| Mara | 22 | 12 | 12 | 0 | 7 | 0 |
| Manyara | 11 | 7 | 3 | 0 | 3 | 1 |
| Mbeya | 17 | 13 | 6 | 0 | 11 | 0 |
| Morogoro | 14 | 6 | 4 | 0 | 4 | 0 |
| Mtwara | 22 | 11 | 4 | 1 | 13 | 0 |
| Mwanza | 23 | 17 | 17 | 2 | 14 | 0 |
| Njombe | 10 | 9 | 9 | 0 | 3 | 0 |
| Pwani | 21 | 19 | 15 | 2 | 6 | 0 |
| Rufiji | 13 | 9 | 8 | 0 | 4 | 0 |
| Rukwa | 6 | 6 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Ruvuma | 23 | 15 | 14 | 0 | 10 | 0 |
| Shinyanga | 7 | 4 | 4 | 0 | 3 | 1 |
| Simiyu | 5 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Singida | 9 | 8 | 12 | 0 | 5 | 0 |
| Songwe | 4 | 4 | 3 | 1 | 3 | 4 |
| Tabora | 12 | 5 | 4 | 0 | 3 | 0 |
| Tanga | 10 | 9 | 7 | 0 | 3 | 0 |
| Tarime - Rorya | 12 | 8 | 6 | 0 | 6 | 0 |
| Wanamaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Reli | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| TAZARA | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Viwanja vya Ndege | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Tanzania Bara** | **583** | **415** | **253** | **8** | **282** | **31** |
| Kaskazini Pemba | 858 | 15 | 5 | 0 | 22 | 2 |
| Kaskazini Unguja | 311 | 14 | 7 | 1 | 12 | 0 |
| Kusini Pemba | 604 | 9 | 8 | 2 | 11 | 2 |
| Kusini Unguja | 469 | 8 | 8 | 2 | 14 | 0 |
| Mjini Magharibi | 1,774 | 44 | 24 | 1 | 34 | 12 |
| **Tanzania Zanzibar** | **4,016** | **90** | **52** | **6** | **93** | **16** |
| **Tanzania** | **4,599** | **505** | **305** | **14** | **375** | **47** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

## 3.3 Vyanzo vya Ajali za Barabarani Tanzania Bara

Vyanzo vikuu vya ajali za barabarani vimegawanyika katika makundi matatu:

i. Sababu za kibinadamu;

ii. Ubovu wa vyombo vya usafiri; na

iii. Sababu za kimazingira.


Jedwali Na. 3.9 linaonesha vyanzo mbalimbali vya ajali kulingana na makundi hayo. Jedwali linaonesha kwamba mwaka 2020 ajali nyingi zaidi zilizotokana na sababu za kibinadamu (ikijumuisha uzembe wa waendesha pikipiki) zilizochangia asilimia 91.6. Ubovu wa vyombo vya usafiri ulichangia asilimia 5.7 na sababu za kimazingira zilichangia asilimia 2.7.

**Jedwali Na. 3.9: Idadi ya Ajali kwa Vyanzo Vyake, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2020**

| | 2016 | | 2019 | | 2020 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Vyanzo vya Ajali kwa Makundi** | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** |
| **Sababu za Kibinadamu** | | | | | | |
| Uendeshaji wa hatari | 496 | 13.3 | 344 | 12.7 | 164 | 9.57 |
| Uzembe wa dereva | 1046 | 28.0 | 816 | 30.2 | 598 | 34.89 |
| Uzembe wa waendesha baiskeli | 103 | 2.8 | 72 | 2.7 | 34 | 1.98 |
| Uzembe wa waendesha pikipiki | 725 | 19.4 | 492 | 18.2 | 307 | 17.91 |
| Uzembe wa abiria | 1 | 0.0 | 6 | 0.2 | 1 | 0.06 |
| Mwendo kasi | 364 | 9.8 | 288 | 10.7 | 272 | 15.87 |
| Mifugo isiyochungwa | 1 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.00 |
| Kupita gari bila uangalifu | 217 | 5.8 | 236 | 8.7 | 97 | 5.66 |
| Uzembe wa watembea kwa miguu | 259 | 6.9 | 162 | 6.0 | 77 | 4.49 |
| Uzembe wa waendesha mikokoteni | 7 | 0.2 | 3 | 0.1 | 5 | 0.29 |
| Ulevi | 61 | 1.6 | 46 | 1.7 | 15 | 0.88 |
| **Jumla** | **3,280** | **87.9** | **2,465** | **91.2** | **1,570** | **91.6** |
| **Ubovu wa Vyombo vya Usafiri** | | | | | | |
| Ubovu wa magari | 197 | 5.3 | 105 | 3.9 | 83 | 4.84 |
| Hitilafu za taa za magari barabarani | 31 | 0.8 | 19 | 0.7 | 15 | 0.88 |
| **Jumla** | **228** | **6.1** | **124** | **4.6** | **98** | **5.7** |
| **Sababu za Kimazingira** | | | | | | |
| Moto | 14 | 0.4 | 10 | 0.4 | 4 | 0.23 |
| Vizuizi vya njia | 120 | 3.2 | 32 | 1.2 | 9 | 0.53 |
| Ubovu wa barabara | 80 | 2.1 | 65 | 2.4 | 30 | 1.75 |
| Vivuko vya reli | 10 | 0.3 | 8 | 0.3 | 3 | 0.18 |
| **Jumla** | **224** | **6.0** | **115** | **4.3** | **46** | **2.7** |
| **Jumla Kuu** | **3,732** | **100** | **2,704** | **100** | **1,714** | **100** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

**Mchoro Na. 9: Vyanzo vya Ajali za Barabarani, Tanzania Bara, Januari – Desemba, 2020**



# SURA YA NNE

## MWELEKEO WA HALI YA UHALIFU

### 4.0 Utangulizi

Takwimu za hali ya uhalifu nchini husaidia kupima utendaji kazi wa Jeshi la Polisi Tanzania kwa kushirikiana na wadau katika kukabiliana na matukio ya uhalifu nchini. Mwelekeo wa hali ya uhalifu hutoa viashiria vinavyoweza kutumika katika kupanga, kusimamia, kufuatilia na kutathmini mipango na programu za muda mfupi, kati na mrefu ili kupambana na uhalifu nchini. Mwelekeo huo huweza pia kurahisisha kazi ya kupanga mipango na kubuni mikakati mipya ya kukabiliana na kupunguza matukio ya uhalifu nchini kwa kiwango kikubwa.

### 4.1 Mwelekeo wa Makosa ya Jinai


Jedwali Na.4.1 linaonesha mwelekeo wa makosa ya jinai katika kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi 2020 (michoro Na. 10a,10b na 10c). Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, takwimu zinaonesha wastani wa makosa makubwa ya jinai kupungua kutoka matukio 75,487 mwaka 2016 hadi matukio 50,689 mwaka 2020. Huu ni upungufu wa makosa 24,798, sawa na asilimia 32.9.

**Jedwali Na. 4.1: Idadi ya Makosa Makubwa na Madogo ya Jinai, Ajali Zilizosababisha Vifo, Vifo na Majeruhi, Tanzania, 2010- 2020**


| Aina ya Kosa | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya Makosa Makubwa ya Jinai** | **76,052** | **72,765** | **73,219** | **70,153** | **68,814** | **75,487** | **67,140** | **60,108** | **58,590** | **50,689** |
| Makosa Dhidi ya Binadamu | 11,049 | 11,206 | 11,335 | 11,166 | 10,698 | 12,567 | 12,578 | 11,759 | 12,223 | 11,001 |
| Makosa ya Kuwania Mali | 50,863 | 46,773 | 45,470 | 43,808 | 40,427 | 40,700 | 33,815 | 29,596 | 27,635 | 24,056 |
| Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii | 14,140 | 14,786 | 16,414 | 15,179 | 17,689 | 22,220 | 20,747 | 18,753 | 17,514 | 14,727 |
| **Jumla ya Makosa Madogo ya Jinai** | **253,354** | **493,937** | **487,232** | **458,422** | **450,389** | **563,787** | **529,393** | **531,695** | **534,281** | **532,556** |
| Makosa Dhidi ya Binadamu | 98,519 | 187,156 | 173,279 | 180,721 | 175,693 | 205,698 | 182,929 | 178,582 | 178,920 | 172,428 |
| Makosa ya Kuwania Mali | 104,455 | 215,070 | 226,011 | 182,024 | 181,104 | 235,804 | 225,598 | 227,623 | 234,663 | 245,230 |
| Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii | 50,380 | 91,711 | 87,942 | 95,677 | 93,592 | 122,285 | 120,866 | 125,490 | 120,698 | 114,898 |
| **Usalama Barabarani** | | | | | | | | | | |
| Matukio Madogo Usalama Barabarani | 441,067 | 603,668 | 663,722 | 1,110,252 | 1,381,705 | 2,200,442 | 2,516,976 | 2,718,732 | 2,311,538 | 2,152,533 |
| Matukio ya Ajali za Barabarani | 24,078 | 23,604 | 24,480 | 15,420 | 8,777 | 10,297 | 6,022 | 3,988 | 2,924 | 1,933 |
| **Jumla Kuu (Makosa ya Jinai na Usalama Barabarani)** | **794,551** | **1,193,974** | **1,248,653** | **1,654,247** | **1,909,685** | **2,850,013** | **3,119,531** | **3,314,523** | **2,907,333** | **2,737,711** |
| Ajali Zilizosababisha Vifo | 3,269 | 3,429 | 3,545 | 3,106 | 2,909 | 2,840 | 2,254 | 1,449 | 1,208 | 1,031 |
| Watu Waliokufa | 4,013 | 4,062 | 4,091 | 3,857 | 3,574 | 3,381 | 2,705 | 1,912 | 1,536 | 1,384 |
| Watu Waliojeruhiwa | 20,917 | 20,037 | 21,536 | 15,259 | 9,993 | 9,549 | 6,169 | 4,194 | 3,123 | 2,362 |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania


**Mchoro Na. 10a: Makosa Makubwa ya Jinai kwa Aina, Tanzania, Januari – Desemba, 2010 – 2020**




**Mchoro Na. 10b: Makosa Makubwa na Madogo ya Jinai, Tanzania, Januari – Desemba, 2010 – 2020**




**Mchoro Na. 10c: Makosa ya Usalama Barabarani Makubwa na Madogo, Tanzania, 2010 – 2020**




## 4.2 Mwelekeo wa Makosa ya Usalama Barabarani

Kwa upande wa usalama barabarani, Jedwali Na. 4.1 na Mchoro Na. 10d kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, takwimu zinaonesha wastani wa matukio makubwa ya usalama barabarani (ajali) kupungua kutoka matukio 10,297 mwaka 2016 hadi matukio 2,924 mwaka 2020. Hali kadhalika makosa madogo ya usalama barabarani kuanzia mwaka 2016 hadi 2018 yaliongezeka kutoka makosa 2,200,442 hadi makosa 2,718,732 mwaka 2018. Hata hivyo makosa madogo ya usalama barabarani yamepungua hadi makosa 2,152,533 mwaka 2020.

**Mchoro Na. 10d: Matukio ya Ajali za Barabarani, Tanzania, 2010 – 2020**



# SURA YA TANO

## OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA

### 5.0 Utangulizi

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeanzishwa kama Ofisi huru ya Umma kupitia Tangazo la Serikali Na.49 la mwaka 2018 la tarehe 13 Februari, 2018 la kuanzisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya kutekeleza mamlaka ya Kikatiba aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye anatoa mchango mkubwa katika kusimamia haki jinai. Kwa mujibu wa Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mkurugenzi wa Mashtaka amepewa uwezo na mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa mashtaka yote ya jinai katika Mahakama zote isipokuwa mahakama za kijeshi. Kwa msingi huo, Mkurugenzi wa Mashtaka ana uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote ya jinai nchini.

Katika kutekeleza majukumu yake, Mkurugenzi wa Mashtaka anatakiwa kufuata kanuni zifuatazo: Kutenda haki; Kuzuia ukiukwaji wa taratibu za kisheria; na kulinda maslahi ya umma. Nafasi hii imewekwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Taifa ya Huduma za Mashtaka, Sura ya 430.

Tangazo la Serikali Na.49 la mwaka 2018 limeweka mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, muundo wake, utawala, ufuatiliaji, usimamizi wa mashtaka na namna ya uratibu na usimamizi wa upelelezi utakavyokuwa kwa lengo la kukuza na kuinua utendaji haki jinai na masuala yanayohusiana nayo.

### 5.1 Majalada Yaliyopokelewa na Kufanyiwa Kazi

Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2020, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipokea jumla ya majalada ya kesi 24,921 kutoka Jeshi la Polisi, Idara ya Upelelezi na Taasisi nyingine za uchunguzi. Baada ya kuzipitia kwa kina kesi zilizokidhi haja ya kisheria na kuandaliwa hati ya mashtaka ni 18,940 ambapo majalada ya kesi 2,009 yalifungwa kwa kukosa ushahidi wa kutosha na majalada ya kesi 4,366 yalirudishwa Polisi kwa ajili ya upelelezi wa kina, kesi ambazo bado zinafanyiwa kazi ni 2,405 (Jedwali Na. 5.1).

**Jedwali Na. 5.1: Majalada Yaliyopokelewa na Kushughulikiwa kutoka Vyombo Chunguzi, Tanzania, 2020**

| Kutoka | Yaliyokuwepo hadi 31 Desemba, 2019 | Yaliyopokelewa | Jumla | Yaliyoandaliwa Mashtaka | Yaliyofungwa | Yaliyorudishwa kwa Upelelezi | Yanayoendelea kufanyiwa kazi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| TAKUKURU | 386 | 206 | 592 | 125 | 296 | 158 | 13 |
| Polisi - Makao Makuu | 87 | 345 | 432 | 95 | 178 | 159 | 0 |
| Polisi - Mkoani - RCOs | 1,057 | 5,518 | 6,575 | 2,939 | 738 | 1,804 | 1,094 |
| Polisi - Wilayani (OC CIDs) | 1,507 | 17,180 | 18,687 | 14,582 | 480 | 2,403 | 1,222 |
| Mamlaka - Dawa za Kulevya | 0 | 747 | 747 | 393 | 270 | 82 | 2 |
| Idara ya Uhamiaji | 5 | 176 | 181 | 121 | 43 | 7 | 13 |
| Taasisi nyingine | 64 | 749 | 813 | 685 | 4 | 63 | 61 |
| **Jumla** | **3,106** | **24,921** | **28,027** | **18,940** | **2,009** | **4,676** | **2,405** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, 2020

## 5.2 Uendeshaji wa Kesi za Jinai

Katika kutekeleza jukumu la uendeshaji wa kesi za jinai, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai zilizosajiliwa katika ngazi ya Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kwa kipindi cha Januarihadi Desemba, 2020 kama inavyoainishwa hapa chini: -

### a) Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya Kesi 34,666 ziliendeshwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi. Kati ya Kesi hizo kesi 11,385 zilikuwa za mwaka 2019 ambayo ni sawa na asilimia 32.9% na kesi 23,245 ambayo ni sawa na asilimia 67.1% zilikuwa ni za mwaka 2020 . Katika kesi zote zilizoshughulikiwa mwaka huu kesi 21,915 zilikwisha Mahakamani na kesi 12,751 bado zinaendelea mahakamani.

**Jedwali Na. 5.2: Kesi zilizoendeshwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi, Tanzania, 2020**

| Aina ya kesi | Zilizovuka 31 Desemba, 2019 | Zilizofunguliwa 2020 | Jumla | Zilizokwisha Mahakamani | Zinazoendelea 2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| Nyara za Serikali | 1,143 | 1024 | 2,167 | 946 | 1,221 |
| Kesi za Maliasili nyinginezo | 81 | 589 | 670 | 606 | 64 |
| Dawa za Kulevya | 1,378 | 2,587 | 3,965 | 2,028 | 1,937 |
| Madini | 55 | 120 | 175 | 102 | 73 |
| Makosa ya Udanganyifu | 536 | 656 | 1192 | 557 | 635 |
| Utakatishaji Fedha | 73 | 107 | 180 | 63 | 117 |
| Unyanganyi wa Kutumia Silaha | 541 | 1031 | 1572 | 787 | 785 |
| Kubaka | 1496 | 3192 | 4688 | 2496 | 2192 |
| Makosa ya Rushwa | 144 | 141 | 285 | 128 | 157 |
| Mauaji (PI) | 1,616 | 1,422 | 3,038 | 1,146 | 1,892 |
| Usalama Barabani | 945 | 6064 | 7009 | 6141 | 868 |
| Jinai za Watoto | 329 | 922 | 1,251 | 883 | 368 |
| Usafirishaji wa Binadamu | 13 | 15 | 28 | 23 | 5 |
| Uhalifu wa Mtandao | 23 | 34 | 57 | 47 | 10 |
| Makosa Mengine | 3,048 | 5,341 | 8,389 | 5,962 | 2,427 |
| **Jumla** | **11,421** | **23,245** | **34,666** | **21,915** | **12,751** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,2020

### b) Mahakama Kuu

Katika ngazi ya Mahakama Kuu, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi katika vikao vya Mahakama Kuu na rufaa na maombi kama ifuatavyo: -

#### (i) Kesi zilizoendeshwa katika vikao vya Mahakama Kuu

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya Kesi 2,294 ziliendeshwa katika ngazi ya Mahakama Kuu. Kati ya Kesi hizo kesi 1,427 zilikuwa za nyuma sawa na asilimia 62.2 na kesi 867 sawa na asilimia 37.8 zilikuwa za mwaka 2020 . Katika kesi zote zilizoshughulikiwa mwaka 2020 kesi 965 zilisikilizwa na kutolewa hukumu na kesi 1,329 zinaendelea mahakamani. (Jedwali Na. 5.3).

**Jedwali Na. 5.3: Kesi zilizoendeshwa Mahakama Kuu**

| Aina ya kesi | Kesi zilizokuwepo hadi kufikia 31 Desemba, 2019 | Kesi zilizofunguliwa | Jumla | Kesi zilizokamilika | Kesi zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|
| Dawa za Kulevya | 163 | 33 | 196 | 57 | 139 |
| Nyara za Serikali | 31 | 29 | 60 | 36 | 24 |
| Utakatishaji Fedha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji ya kukusudia | 1,128 | 716 | 1,844 | 760 | 1,084 |
| Mauaji yasiyo ya kukusudia | 84 | 81 | 165 | 93 | 72 |
| Makosa Mengineyo | 21 | 8 | 29 | 19 | 10 |
| **Jumla** | **1,427** | **867** | **2,294** | **965** | **1,329** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,2020

#### (ii) Kesi zilizoendeshwa katika Mahakama Kuu- Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya Kesi **49** ziliendeshwa katika Mahakama Kuu-Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Kati ya Kesi hizo kesi 7 zilikuwa za nyuma sawa na asilimia 14.3% na kesi 42 sawa na asilimia 85.7% zilikuwa za mwaka 2020. Katika kesi zote zilizoshughulikiwa mwaka 2020 kesi **13** zilisikilizwa na kutolewa maamuzi na kesi **36** zilikuwa zinaendelea mahakamani. (Jedwali Na. 5.4).

**Jedwali Na. 5.4: Idadi ya Kesi zilizofunguliwa na kuisha katika Mahakama Kuu –Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi**

| Kesi | Zilizkuwepo hadi kufikia 31 Desemba, 2019 | Zilizofunguliwa | Jumla | Zilizokamilika | Kifungo | Kuachiwa Huru | Nolle | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uhujumu Uchumi | 2 | 26 | 28 | 11 | 6 | 3 | 2 | 17 |
| Maombi (Applications) | 5 | 16 | 21 | 2 | - | - | - | 19 |
| **Jumla** | **7** | **42** | **49** | **13** | **6** | **3** | **2** | **36** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,2020

## 5.3 Ukamilishaji wa Kesi za Jinai

### a) Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi

Jumla Jumla ya kesi 24,365 zilikwisha Mahakamani, ambapo kesi 13,403 washtakiwa walitiwa hatiani, kesi 2,155 , washtakiwa waliachiwa huru, kesi 1,970 ziliondolewa chini ya kifungu cha 98(a) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Waendesha Mashtaka waliokasimiwa mamlaka ya kuendesha Kesi na kesi 1,633 ziliondolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kifungu 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 kutokana na ushahidi kuwa hafifu, Kesi 4,457 zilifutwa na Mahakama chini ya vifungu vya 225(5), 222 na 226 vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwa sababu mbalimbali kama vile upelelezi kutokamilika au mashahidi kutohudhuria mahakamani na mapungufu ya Kiutendaji ya wadau wa Haki Jinai. Vilevile kesi 697 zilikamilishwa na kupelekwa Mahakama Kuu kwa ajili ya kusikilizwa, na kesi 50 washitakiwa walifariki kabla ya kesi kukamilika. (Jedwali Na. 5.5 na 5.6).

**Jedwali Na. 5.5: Jinsi kesi Zilivyokwisha katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi**

| Aina ya kesi | Watuhumiwa kutiwa hatiani | Kesi ziliziondolewa na Waendesha Mashtaka chini ya k/f 98 (a) CPA | Kesi zilizofutwa na Mahakama chini ya k/f225 (5) CPA | Kesi zilizoondolewa na Mawakili wa Serikali chini ya k/f 91(1) CPA | Watuhumiwa kuachiwa huru | Kesi zilizokamilishwa kwenda Mahakama Kuu | Kesi zilizofutwa chini ya k/f 222 & 226 CPA | Kesi ambazo zimeondolewa kwa washitakiwa kufariki k/f 224A CPA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nyara za Serikali | 639 | 67 | 94 | 79 | 65 | 0 | 3 | 3 |
| Kesi za Maliasili nyinginezo | 433 | 12 | 89 | 12 | 29 | 0 | 0 | 0 |
| Madawa ya Kulevya | 1246 | 92 | 762 | 144 | 150 | 0 | 4 | 3 |
| Madini | 74 | 5 | 12 | 12 | 25 | 0 | 1 | 1 |
| Makosa ya Udanganyifu | 198 | 37 | 155 | 42 | 79 | 0 | 1 | 3 |
| Utakatishaji Fedha | 46 | 5 | 6 | 11 | 6 | 0 | 1 | 1 |
| Unyanganyi wa Kutumia Silaha | 297 | 54 | 308 | 49 | 179 | 0 | 4 | 1 |
| Kubaka | 1162 | 201 | 1204 | 82 | 378 | 0 | 15 | 5 |
| Makosa ya Rushwa | 27 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji (PI) | 0 | 0 | 0 | 472 | 0 | 697 | 0 | 15 |
| Usalama Barabani | 5276 | 265 | 204 | 54 | 241 | 0 | 0 | 0 |
| Jinai za Watoto | 664 | 65 | 219 | 25 | 64 | 0 | 1 | 3 |
| Makosa Mengine | 3330 | 1157 | 1358 | 644 | 935 | 0 | 8 | 15 |
| **Jumla** | **13,403** | **1970** | **4419** | **1633** | **2155** | **697** | **38** | **50** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,2020

### b) Mahakama Kuu

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2020, jumla ya kesi 965 zilifanyiwa kazi. Ambapo watuhumiwa 536 walitiwa hatiani na Watuhumiwa 176 waliachiwa huru. Kesi 213 ziliondolewa na mawakili wa serikali chini ya kifungu 91(1) cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai na kesi 11 zilifutwa kutokana na watuhumiwa kufariki na Watuhumiwa 26 walipelekwa kwenye taasisi ya afya ya akili (Criminal Lunatic) (Jedwali Na. 5.6).

**Jedwali Na. 5.6: Kesi zilivyokamilika Mahakama Kuu**

| Aina ya kesi | Watuhumiwa kutiwa hatiani | Watuhumiwa kuachiwa huru | Kesi zilizoondolewa na Mawakili wa Serikali chini ya k/f 91(1) CPA | Watuhumiwa kuamriwa kupelekwa kwenye taasisi ya afya ya akili (Criminal Lunatic) | Kesi zilizofutwa kutokana na watuhumiwa kufariki |
|---|---|---|---|---|---|
| Dawa za Kulevya | 34 | 13 | 10 | 0 | 0 |
| Nyara za Serikali | 26 | 7 | 3 | 0 | 0 |
| Mauaji ya kukusudia | 392 | 144 | 187 | 26 | 11 |
| Mauaji yasiyo ya kukusudia | 74 | 12 | 7 | 0 | 0 |
| Makosa Mengineyo | 10 | 3 | 6 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **536** | **179** | **213** | **26** | **11** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,2020

### c) Faini na Mali zilizotaifishwa

Washtakiwa waliotiwa hatiani kutokana na kesi za jinai walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo vifungo, faini na mali mbalimbali kutaifishwa. Kiasi cha zaidi ya TZS 1,000,000,000.00 kililipwa Mahakamani kama faini katika kesi 1500. Mali na fedha zinazokadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya TZS 50,000,000,000.00 zilitaifishwa kwa amri ya Mahakama. Baadhi ya mali hizo ni pamoja na fedha taslimu, madini, injini za boti, magari, nyumba, viwanja, mashamba, pikipiki, baiskeli, magogo na mbao.

## 5.4 Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Upelelezi

Pamoja na kuratibu upelelezi kwa kupitia majalada yaliwasilishwa na vyombo chunguzi na kutoa maelekezo stahiki, Ofisi imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli mbalimbali za upelelezi kwa kuchukua hatua mahususi kama ifuatavyo: -

### (a) Uundwaji wa vikosi kazi maalum kusimamia upelelezi

Uratibu na usimamizi wa upelelezi ulifanyika katika kipindi husika katika matukio makubwa yaliyohitaji maelekezo kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kuboresha ushahidi. Lengo kubwa la kuratibu upelelezi ni kuhakikisha Ofisi yetu inashirikiana kwa ukaribu na vyombo chunguzi ili kuboresha ushahidi na hivyo kuleta matokeo chanya pindi kesi zinapowasilishwa Mahakamani. Vile vile, Ofisi ilendelea kushirikiana na vyombo chunguzi katika harakati za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuchukua hatua za kisheria ikiwemo mashtaka kwa wakosaji.

### (b) Vikao na Wapelelezi

Vikao vya mara kwa mara vilifanyika kati ya Mawakili wa Serikali na Wapelelezi. Lengo la vikao hivyo ilikuwa ni kujadili upungufu wa kiushahidi katika majalada yaliyowasilishwa katika ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua za kimashtaka na kupata maelekezo ya namna ya kurekebisha upungufu huo. Vikao hivi vilifanyika katika ngazi ya Makao Makuu ya Upelelezi, Mikoa na Wilaya kulingana na mahitaji ya kesi husika.

# SURA YA SITA

## TAARIFA YA WAFUNGWA WALIOPOKELEWA MAGEREZANI NA WALIONUFAIKA NA MSAMAHA WA RAIS

### 6.0 Utangulizi

Jeshi la Magereza Tanzania Bara lilianzishwa kwa mujibu wa sheria Na. 34 ya Mwaka 1967 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002. Pia zipo sheria na Kanuni nyingine za uendeshaji wa Jeshi la Magereza za Mwaka 1968 na marekebisho yake. Jeshi la Magereza lina jukumu la kuwapokea na kuwahifadhi wahalifu wa aina zote wanaoletwa gerezani kwa mujibu wa Sheria. Pia, kuandaa programu mbalimbali zenye lengo la kuwarekebisha wahalifu ili watokapo gerezani wawe raia wema.

### 6.1 Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani

Mwaka 2020 wafungwa waliopokelewa magerezani walikuwa 29,764 kati yao watu wazima walikuwa 29, 282 (wanaume 27,414, wanawake 1,868) na vijana 482. Mikoa inayoongoza kupokea wafungwa wengi ni Kagera (2,301), Mwanza (2,186), Dar es Salaam (2,168), Kigoma (2,163) na Morogoro (2,088), Wengi wa wafungwa ni wale wenye miaka 26–50, ambao walikuwa 15,240 sawa na asilimia 51.2 Mikoa iliyopokea wafungwa wengi wa umri huo kuliko mikoa mingine ni Kagera ulipokea wafungwa (1,325; asilimia 4.5), Mwanza (1,250; asilimia 4.2) na Mbeya (1,161; asilimia 3.9). Aidha, mikoa iliyopokea wafungwa wachache wa umri huo kuliko mikoa mingine ni Geita (45; asilimia 0.15), Katavi (59; asilimia 0.16) na Njombe (59; asilimia 0.20). (Jedwali Na. 6.1).

**Jedwali Na. 6.1: Idadi ya Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Umri, Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2020**

| Mkoa | Vijana | Watu Wazima | | | | | | | | | | | | Jumla kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Miaka 15-17 | Miaka 18_20 | | | Miaka 21- 25 | | | Miaka 26 - 50 | | | Zaidi ya miaka 50 | | | |
| | | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | |
| Arusha | 1 | 103 | 9 | 112 | 214 | 28 | 242 | 226 | 21 | 247 | 45 | 2 | 47 | **649** |
| Dar es Salaam | 0 | 499 | 54 | 553 | 459 | 95 | 554 | 895 | 71 | 966 | 75 | 20 | 95 | **2,168** |
| Dodoma | 17 | 234 | 7 | 241 | 360 | 28 | 388 | 650 | 63 | 713 | 69 | 2 | 71 | **1,430** |
| Geita | 0 | 18 | 1 | 19 | 29 | 7 | 36 | 43 | 2 | 45 | 11 | 0 | 11 | **111** |
| Iringa | | 216 | 2 | 218 | 356 | 13 | 369 | 445 | 35 | 480 | 60 | 4 | 64 | **1,131** |
| Kagera | 19 | 287 | 8 | 295 | 494 | 50 | 544 | 1,225 | 100 | 1325 | 108 | 10 | 118 | **2,301** |
| Katavi | 0 | 21 | 1 | 22 | 32 | 2 | 34 | 48 | 1 | 49 | 19 | 2 | 21 | **126** |
| Kigoma | 57 | 494 | 5 | 499 | 539 | 15 | 554 | 933 | 42 | 975 | 65 | 13 | 78 | **2,163** |
| Kilimanjaro | 9 | 203 | 9 | 212 | 305 | 29 | 334 | 427 | 46 | 473 | 87 | 10 | 97 | **1,125** |
| Lindi | | 98 | 1 | 99 | 136 | 6 | 142 | 435 | 29 | 464 | 13 | | 13 | **718** |
| Manyara | 8 | 138 | 4 | 142 | 219 | 8 | 227 | 494 | 38 | 532 | 55 | 2 | 57 | **966** |
| Mara | 51 | 154 | 9 | 163 | 278 | 18 | 296 | 732 | 53 | 785 | 96 | 8 | 104 | **1,399** |
| Mbeya | 7 | 231 | 22 | 253 | 424 | 32 | 456 | 1,095 | 66 | 1161 | 68 | 11 | 79 | **1,956** |
| Morogoro | 126 | 200 | 13 | 213 | 543 | 28 | 571 | 1,038 | 63 | 1101 | 71 | 6 | 77 | **2,088** |
| Mtwara | 3 | 270 | 3 | 273 | 239 | 3 | 242 | 382 | 14 | 396 | 18 | 1 | 19 | **933** |
| Mwanza | 129 | 284 | 14 | 298 | 371 | 44 | 415 | 1,165 | 85 | 1250 | 83 | 11 | 94 | **2,186** |
| Njombe | 0 | 35 | 3 | 38 | 56 | 54 | 110 | 54 | 5 | 59 | 9 | 1 | 10 | **217** |
| Pwani | 9 | 289 | 4 | 293 | 421 | 3 | 424 | 482 | 13 | 495 | 26 | 2 | 28 | **1,249** |
| Ruvuma | 4 | 197 | 8 | 205 | 265 | 15 | 280 | 423 | 20 | 443 | 25 | 2 | 27 | **959** |
| Rukwa | 19 | 93 | 12 | 105 | 185 | 7 | 192 | 374 | 31 | 405 | 19 | 3 | 22 | **743** |
| Singida | 8 | 74 | 3 | 77 | 198 | 12 | 210 | 491 | 41 | 532 | 43 | 1 | 44 | **871** |
| Simiyu | 1 | 42 | 3 | 45 | 38 | 1 | 39 | 59 | 1 | 60 | 11 | | 11 | **156** |
| Shinyanga | 3 | 226 | 13 | 239 | 197 | 13 | 210 | 535 | 36 | 571 | 31 | 1 | 32 | **1,055** |
| Songwe | 2 | 27 | 3 | 30 | 24 | 5 | 29 | 94 | 3 | 97 | 18 | | 18 | **176** |
| Tabora | | 176 | 12 | 188 | 380 | 18 | 398 | 724 | 38 | 762 | 83 | 1 | 84 | **1,432** |
| Tanga | 9 | 187 | 4 | 191 | 286 | 15 | 301 | 801 | 53 | 854 | 92 | 9 | 101 | **1,456** |
| **Jumla** | **482** | **4,796** | **227** | **5,023** | **7,048** | **549** | **7597** | **14,270** | **970** | **15,240** | **1,300** | **122** | **1,422** | **29,764** |

Chanzo: Jeshi la Magereza, Tanzania Bara

## 6.2 Wafungwa Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani

Mwaka 2020 wafungwa watu wazima 29,282 walipokelewa magerezani kutoka mahakamani. Wengi wao walikutwa na hatia ya makosa ya Wizi (7,908; asilimia 27.0), Kuvunja na Kuiba (2,674; asilimia 9.1) na Kujeruhi (2,413; asilimia 8.0) na makosa ambayo yalikuwa na wafungwa wachache ni Kuchoma nyumba moto (312; asilimia 1.1), Mauaji (328; asilimia 1.1) na Kupatikana na silaha/risasi (527; asilimia 1.8). (Jedwali Na.6.2).

**Jedwali Na. 6.2: Idadi ya Wafungwa Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2020**

| Aina ya Kosa | Chini ya miezi 6 | | Zaidi ya miezi 6 - mwaka 1 | | Zaidi ya mwaka 1-3 | | Zaidi ya miaka 3-5 | | Zaidi ya miaka 5-10 | | Zaidi ya miaka 10-15 | | Zaidi ya miaka 15- 20 | | Zaidi ya miaka 20- 30 | | Zaidi ya maika 30 | | Kifungo cha maisha | | Hukumu ya kunyongwa | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | |
| Mauaji | 48 | 8 | 15 | 6 | 56 | 8 | 44 | 5 | 47 | 0 | 16 | 0 | 5 | 0 | 3 | 0 | | 0 | 22 | 0 | 65 | 2 | **350** |
| Kuua bila kukusudia | 59 | 2 | 54 | 2 | 109 | 14 | 89 | 13 | 105 | 8 | 53 | 0 | 24 | 0 | 0 | 0 | 18 | 0 | 8 | 2 | 0 | 0 | **560** |
| Kujaribu kuua | 129 | 1 | 136 | 0 | 144 | 1 | 124 | 1 | 43 | 1 | 22 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **602** |
| Unyang'anyi | 108 | 5 | 205 | 12 | 144 | 12 | 156 | 0 | 133 | 0 | 139 | 1 | 112 | 0 | 296 | 0 | 45 | 0 | 3 | | 0 | 0 | **1,371** |
| Wizi | 2,714 | 202 | 2,130 | 108 | 2,132 | 96 | 119 | 14 | 241 | 12 | 40 | 0 | 41 | 0 | 29 | 0 | 30 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **7,908** |
| Kuvunja na kuiba | 521 | 34 | 734 | 46 | 765 | 26 | 234 | 18 | 146 | 0 | 65 | 2 | 24 | 0 | 26 | 0 | 33 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2,674** |
| Kupatikana na dawa za kulevya | 94 | 8 | 181 | 3 | 109 | 3 | 111 | 3 | 65 | 0 | 49 | 0 | 19 | 0 | 12 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **658** |
| Kupatikana na nyara za serikali | 85 | 3 | 77 | 5 | 201 | 7 | 2 | 2 | 45 | 1 | 1 | 0 | 108 | 0 | 25 | 0 | 1 | 0 | 17 | 4 | 0 | 0 | **584** |
| Makosa ya kujamiiana | 37 | 5 | 157 | 3 | 271 | 6 | 0 | 0 | 55 | 0 | 24 | 0 | 33 | 0 | 282 | 0 | 25 | 0 | 193 | 0 | 0 | 0 | **1,091** |
| Kupatikana na silaha/risasi | 88 | 0 | 122 | 0 | 71 | 1 | 65 | 0 | 78 | 0 | 37 | 0 | 21 | 0 | 24 | 0 | 20 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **527** |
| Kujeruhi | 627 | 65 | 820 | 88 | 681 | 34 | 7 | 14 | 40 | 15 | 22 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2,413** |
| Kuchoma nyumba moto | 77 | 17 | 88 | 14 | 35 | 9 | 22 | 0 | 27 | 0 | 14 | 0 | 8 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **312** |
| Rushwa | 165 | 22 | 209 | 15 | 156 | 12 | 112 | 0 | 76 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **767** |
| Kupatikana na pombe haramu ya moshi | 346 | 30 | 236 | 30 | 123 | 7 | 35 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **808** |
| Uzembe na uzururaji | 678 | 86 | 195 | 28 | 251 | 22 | 125 | 0 | 87 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1,472** |
| Makosa mengineyo | 2,118 | 98 | 1,931 | 95 | 1,628 | 44 | 642 | 46 | 324 | 18 | 120 | 1 | 68 | 0 | 1 | 290 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **7,428** |
| **Jumla** | **7,894** | **586** | **7,290** | **455** | **6,876** | **302** | **1,887** | **117** | **1,512** | **55** | **602** | **4** | **463** | **0** | **699** | **291** | **176** | **0** | **243** | **6** | **65** | **2** | **29,282** |

Chanzo: Jeshi la Magereza, Tanzania Bara

### 6.3 Wafungwa Vijana Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani

Mwaka 2020, wafungwa vijana 482 walipokelewa magerezani kutoka mahakamani ambapo wanaume walikuwa 421 na wanawake 61. Wengi wao walihukumiwa kwa makosa ya Wizi (112; asilimia 23.2), Kujeruhi (73; asilimia 15.1) na Kuvunja na Kuiba (71; asilimia 14.7). Makosa yaliyokuwa na wafungwa wachache ni Kujaribu Kuua (2; asilimia 0.4), Mauaji (4; asilimia 0.8) na Kuchoma nyumba moto (5; asilimia 1.0). Wafungwa vijana walifungwa zaidi vifungo vya chini ya miezi 6 mpaka miaka 5 kulingana na aina ya kosa. (Jedwali Na 6.3).

**Jedwali Na. 6.3: Idadi ya Wafungwa Vijana Waliopokolewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2020**

| Aina ya Kosa | Chini ya miezi 6 | | Zaidi ya miezi 6 - mwaka 1 | | Zaidi ya mwaka 1-3 | | Zaidi ya miaka 3 hadi 5 | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | **4** |
| Kuua bila kukusudia | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 1 | 0 | 0 | **6** |
| KujaribuKujaribu kuua | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2** |
| Unyang'anyi | 0 | 0 | 4 | 0 | 5 | 0 | 2 | 0 | **11** |
| Wizi | 52 | 4 | 28 | 4 | 13 | 0 | 11 | 0 | **112** |
| Kuvunja na kuiba | 25 | 2 | 8 | 3 | 20 | 1 | 10 | 2 | **71** |
| Kupatikana na dawa za kulevya | 2 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | **8** |
| Kupatikana na nyara za serikali | 2 | 0 | 4 | 1 | 5 | 1 | 0 | 0 | **13** |
| Kujamiiana | 19 | 7 | 17 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | **45** |
| Kujeruhi | 32 | 5 | 14 | 3 | 17 | 2 | 0 | 0 | **73** |
| Kuchoma nyumba moto | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 0 | 0 | **5** |
| Rushwa | 0 | 0 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **9** |
| Kupatikana na pombe haramu ya moshi | 5 | 3 | 8 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | **18** |
| Uzembe na uzururaji | 5 | 2 | 1 | 2 | 7 | 0 | 0 | 0 | **17** |
| Makosa mengineyo | 31 | 7 | 15 | 2 | 21 | 3 | 9 | 0 | **88** |
| **Jumla** | **173** | **30** | **114** | **19** | **101** | **10** | **33** | **2** | **482** |

Chanzo: Jeshi la Magereza, Tanzania Bara

### 6.4 Wafungwa Walionufaika na Msamaha na Aina ya Makosa

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 45(1)(a-d) inampa Rais mamlaka ya kumsamehe mfungwa kwa amri au bila sababu, makosa au madai yote yanayohusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msamaha huo hutolewa kila mwaka kwa wafungwa ambao wataonekana kuwa na sifa.

Sifa zinazopewa kipaumbele kwa wafungwa kupata msamaha ni zifuatazo: -

i. Wafungwa wote ambao baada ya punguzo la kawaida la moja ya tatu (1/3) linalotolewa chini ya Kifungu 49(1) cha Sheria ya Magereza Sura ya 58, watakuwa wametumikia nusu (½) ya vifungo vyao vilivyobaki, isipokuwa wafungwa walioorodheshwa katika Ibara ya 2(i – xxi);
ii. Wafungwa wagonjwa wenye magonjwa kama UKIMWI, kifua kikuu na saratani;
iii. Wafungwa wazee wenye umri wa miaka sabini (70) au zaidi;
iv. Wafungwa wa kike walioingia na mimba gerezani, pamoja na wale walioingia na watoto wanaonyonya na wasionyonya; na
v. Wafungwa wenye ulemavu wa mwili na akili.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia madaraka aliyopewa chini ya Ibara ya 45(1)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 2020 alitoa msamaha kwa wafungwa 7,036 ambapo kati yao 5,105 sawa na asilimia 72.6 ya waliosamehewa, walipunguziwa vifungo vyao na 1,931 sawa na asilimia 27.4 waliachiliwa huru. Msamaha huo wa wafungwa ulitolewa wakati wa maadhimisho ya miaka 56 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 April 2020 na Maadhimisho ya miaka 59 ya uhuru wa Tanganyika tarehe 9, Disemba 2020.

Katika maadhimisho ya sherehe ya Muungano, Mheshimiwa Rais alitoa msamaha kwa wafungwa 3,717 kati yao 2,786 walipunguziwa vifungo vyao na 931 waliachiliwa huru na katika maadhimisho ya sherehe ya Uhuru alitoa msamaha kwa wafungwa 3,319 kati yao 2,319 walipunguziwa vifungo vyao na 1,000 waliachiliwa huru.

Mikoa iliyoongoza kuwa na wafungwa wengi walioachiwa huru ni Geita 191 sawa na asilimia 9.9, Kigoma 178 sawa na asilimia 9.2 na Dar es salaam 151 sawa na asilimia 7.8. Mikoa iliyokuwa na wafungwa wachache walioachiliwa huru ni Iringa 20 sawa na asilimia 1.0, Manyara 24 sawa na asilimia 1.2 na Njombe 27 sawa na asilimia 1.4 (Jedwali Na. 6.4).

Aidha kwa mamlaka aliyopewa Mheshimiwa Rais katika Ibara ya 45(1)(a-d) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 2020 aliwabadilishia adhabu wafungwa 256 wa kunyongwa na kuwa wafungwa wa maisha.

**Jedwali Na. 6.4: Idadi ya Wafungwa Walioachiwa Huru kwa Aina ya Kosa na Mkoa , Tanzania Bara, 2020**

| Mkoa | Msamaha April 26,2020 | | | Msamaha Disemba 9,2020 | | | Jumla Ya Waliopunguziwa Vifungo | Jumla Ya Walioachiliwa | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Waliopunguziwa Vifungo | Walioachiliwa Huru | Jumla | Waliopunguziwa Vifungo | Walioachiliwa | Jumla | | | |
| Arusha | 78 | 27 | 105 | 47 | 26 | 73 | 125 | 53 | **178** |
| Dar Es Salaam | 156 | 95 | 251 | 185 | 56 | 241 | 341 | 151 | **492** |
| Dodoma | 146 | 25 | 171 | 115 | 25 | 140 | 261 | 50 | **311** |
| Geita | 173 | 104 | 277 | 155 | 87 | 242 | 328 | 191 | **519** |
| Iringa | 78 | 6 | 84 | 62 | 14 | 76 | 140 | 20 | **160** |
| Kagera | 350 | 73 | 423 | 236 | 52 | 288 | 586 | 125 | **711** |
| Katavi | 78 | 27 | 105 | 69 | 16 | 85 | 147 | 43 | **190** |
| Kigoma | 121 | 60 | 181 | 90 | 118 | 208 | 211 | 178 | **389** |
| Kilimanjaro | 69 | 42 | 111 | 77 | 40 | 117 | 146 | 82 | **228** |
| Lindi | 46 | 16 | 62 | 54 | 26 | 80 | 100 | 42 | **142** |
| Manyara | 40 | 8 | 48 | 55 | 16 | 71 | 95 | 24 | **119** |
| Mara | 136 | 46 | 182 | 115 | 42 | 157 | 251 | 88 | **339** |
| Mbeya | 145 | 29 | 174 | 129 | 51 | 180 | 274 | 80 | **354** |
| Morogoro | 194 | 47 | 241 | 246 | 75 | 321 | 440 | 122 | **562** |
| Mtwara | 67 | 21 | 88 | 46 | 18 | 64 | 113 | 39 | **152** |
| Mwanza | 112 | 49 | 161 | 84 | 46 | 130 | 196 | 95 | **291** |
| Njombe | 69 | 11 | 80 | 40 | 16 | 56 | 109 | 27 | **136** |
| Pwani | 112 | 40 | 152 | 81 | 68 | 149 | 193 | 108 | **301** |
| Rukwa | 127 | 16 | 143 | 66 | 17 | 83 | 193 | 33 | **226** |
| Ruvuma | 76 | 20 | 96 | 37 | 16 | 53 | 113 | 36 | **149** |
| Shinyanga | 43 | 15 | 58 | 31 | 17 | 48 | 74 | 32 | **106** |
| Simiyu | 66 | 17 | 83 | 58 | 19 | 77 | 124 | 36 | **160** |
| Singida | 42 | 29 | 71 | 42 | 21 | 63 | 84 | 50 | **134** |
| Songwe | 60 | 21 | 81 | 45 | 21 | 66 | 105 | 42 | **147** |
| Tabora | 88 | 41 | 129 | 82 | 26 | 108 | 170 | 67 | **237** |
| Tanga | 114 | 46 | 160 | 72 | 71 | 143 | 186 | 117 | **303** |
| **Jumla** | **2,786** | **931** | **3,717** | **2,319** | **1,000** | **3,319** | **5,105** | **1,931** | **7,036** |

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

# SURA YA SABA

# UHUSIANO KATI YA UHALIFU NA VIGEZO VYA KIJAMII NA KIUCHUMI

## 7.0 Utangulizi

Sura hii inaangalia uhusiano uliopo baina ya makosa mbalimbali na vigezo vya kijamii, kiuchumi na utandawazi ambavyo vimekuwa vikipelekea kuongezeka kwa idadi ya uhalifu nchini kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020. Baadhi ya vigezo hivyo ni kama vile idadi ya watu, eneo la ardhi na idadi ya askari. Tafiti mbalimbali zilizofanyika zinaonesha kuwa, kuna uhusiano mkubwa kati ya uhalifu na hali ya maisha ya watu pamoja na mazingira. Matokeo ya tafiti hizo yameliwezesha Jeshi la Polisi kubaini mbinu mbalimbali pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kupambana na kukomesha hali ya uhalifu nchini.

## 7.1 Uhusiano wa Uhalifu na Masuala ya Kijamii na Kiuchumi

Upo uhusiano wa karibu kati ya makosa yanayotendeka na idadi ya watu nchini,uhusiano huu kwa kawaida ni chanya, hii ina maanisha kuwa, mikoa yenye idadi kubwa ya watu ina idadi kubwa ya makosa tofauti na mikoa yenye watu wachache. Kutokana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi, 2012 makisio ya idadi ya watu kwa mwaka 2020 ni 57,637,628 na makosa ya jinai yaliyoripotiwa ni 583,245, Dar es Salaam (watu 5,781,557, Makosa 139,835) Mwanza ( watu 3,217,328, makosa 50,167), Kilimanjaro (watu 1,790,113 , Makosa 34,161 ), Morogoro (watu 2,495,462, makosa 31,761) na Mbeya (watu 2,136,614, makosa 24,274), (Jedwali Na. 45).

Kwa upande mwingine, idadi ya askari inapokuwa kubwa inasaidia kuwepo kwa amani na utulivu ambao utawezesha watu kutumia muda wao vizuri katika shughuli za uzalishaji mali na ufanyaji wa biashara ili kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. Hii itasaidia kupunguza kasi ya umaskini na kuleta maendeleo kwa Taifa.

Upo uhusiano kati ya umaskini na ongezeko la uhalifu, umaskini unapoongezeka hupelekea kuongezeka kwa uhalifu hii inatokana na kukosekana kwa kipato na kusababisha kuwepo kwa ongezeko la matukio ya uhalifu kwani watu hutumia njia zisizo halali ili kujipatia kipato.

## 7.2 Uhusiano wa Makosa ya Jinai na Idadi ya Watu, Eneo la Ardhi na Jeshi la Polisi

### 7.2.1 Uwiano wa Askari na Idadi ya Watu

Idadi ya watu wanao hudumiwa na askari polisi mmoja inaoneshwa na uwiano wa idadi ya askari na idadi ya watu. Kulingana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi Tanzania kwa mwaka 2012, makisio ya idadi ya watu kwa mwaka 2020 ni 57,637,628 hivyo askari mmoja anahudumia watu 1,293 (1:1,293). Kulingana na viwango vya kimataifa, askari mmoja anatakiwa kuhudumia si zaidi ya watu 450 (UN - ISCCJ 2011 Report[1]). Hii ina maana kuwa askari polisi wa Tanzania ana mzigo mkubwa ni

[1]UN - United Nations report on International Statistics on Crime and Criminal Justice.

mara tatu ya ule uliopendekezwa kimataifa. Ili kukidhi viwango vya kimataifa, Jeshi la Polisi linahitaji kuajiri angalau mara mbili zaidi ya idadi ya askari waliokuwepo mwaka 2020.

Jedwali Na. 7.1 linaonesha uwiano kati ya idadi ya watu na askari, makosa ya jinai kwa kila mkoa na idadi ya askari kwa kila eneo la kilometa 100 za mraba kimkoa. Mikoa inayoongoza kuwa na uwiano mkubwa wa watu kwa askari ni Simiyu (1:3,465), Tabora (1:2,768), Geita (1:2,457), Songwe (1:2,417), na Kigoma (1:2,342). Mikoa yenye uwiano mdogo ni Kusini Unguja (1:269), Mjini Magharibi (1:287) na, Kaskazini Unguja (1:537).

**Jedwali Na. 7.1: Uwiano Kati ya Idadi ya Watu na Askari, Makosa ya Jinai kwa kila Askari na Idadi ya Askari kwa Kila Kilomita 100 za Mraba Kimkoa, Tanzania, Januari - Desemba, 2020**

| Mkoa | Makosa ya Jinai | Idadi ya Watu | Eneo (kilomita za Mraba) | Watu / Askari | Askari / kilomita za Mraba 100 | Makosa ya Jinai / Askari |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 26,767 | 2,104,074 | 37,576 | 1,858 | 1,132 | 5 |
| Dar es Salaam | 140,285 | 5,401,814 | 1,393 | 7,277 | 742 | 522 |
| Dodoma | 23,101 | 2,647,410 | 41,311 | 2,378 | 1,113 | 6 |
| Geita | 18,939 | 2,434,800 | 20,054 | 991 | 2,457 | 5 |
| Iringa | 11,424 | 1,149,481 | 35,503 | 1,060 | 1,084 | 3 |
| Kagera | 17,944 | 3,238,347 | 25,265 | 1,422 | 2,277 | 6 |
| Katavi | 8,371 | 805,887 | 45,843 | 563 | 1,431 | 1 |
| Kigoma | 12,221 | 2,800,919 | 37,040 | 1,196 | 2,342 | 3 |
| Kilimanjaro | 30,196 | 1,951,252 | 13,250 | 1,613 | 1,210 | 12 |
| Lindi | 6,841 | 1,025,800 | 66,040 | 857 | 1,197 | 1 |
| Manyara | 12,524 | 1,672,386 | 44,522 | 1,024 | 1,633 | 2 |
| Mara | 12,562 | 1,873,105 | 21,760 | 1,104 | 1,697 | 5 |
| Mbeya | 22,806 | 2,204,543 | 37,719 | 1,417 | 1,556 | 4 |
| Morogoro | 27,438 | 2,730,058 | 70,624 | 1,848 | 1,477 | 3 |
| Mtwara | 10,009 | 1,478,874 | 16,710 | 1,071 | 1,381 | 6 |
| Mwanza | 49,454 | 3,826,573 | 9,467 | 1,869 | 2,047 | 20 |
| Njombe | 8,694 | 837,557 | 21,347 | 716 | 1,170 | 3 |
| Pwani | 14,579 | 749,580 | 32,547 | 1,022 | 733 | 3 |
| Rufiji | 6,090 | 576,272 | | 563 | 1,024 | NA |
| Rukwa | 9,616 | 1,270,049 | 22,792 | 836 | 1,519 | 4 |
| Ruvuma | 11,098 | 1,655,443 | 63,669 | 1,014 | 1,633 | 2 |
| Shinyanga | 15,031 | 1,993,589 | 18,901 | 1,044 | 1,910 | 6 |
| Simiyu | 7,338 | 2,304,228 | 25,212 | 665 | 3,465 | 3 |
| Singida | 13,243 | 1,705,182 | 49,340 | 1,051 | 1,622 | 2 |
| Songwe | 8,019 | 1278850 | 22,631 | 529 | 2,417 | 2 |
| Tabora | 16,289 | 3,081,263 | 76,150 | 1,113 | 2,768 | 1 |
| Tanga | 20,714 | 2,449,235 | 26,677 | 1,462 | 1,675 | 5 |
| Tarime - Rorya | 12,334 | 719459 | NA | 789 | 912 | NA |
| Vikosi | 726 | NA | NA | 1,961 | | NA |
| **Tanzania Bara** | **574,653** | **55,966,030** | **883,343** | **40,313** | **1,388** | **5** |
| Kaskazini Unguja | 719 | 232,480 | 470 | 433 | 537 | 92 |
| Kusini Unguja | 871 | 138,589 | 854 | 516 | 269 | 60 |
| Mjini Magharibi | 5,224 | 733,914 | 230 | 2,557 | 287 | 1,112 |
| Kaskazini Pemba | 871 | 294,267 | 574 | 408 | 721 | 71 |
| Kusini Pemba | 907 | 272,348 | 332 | 352 | 774 | 106 |
| **Tanzania Zanzibar** | **8,592** | **1,671,598** | **2,460** | **4,266** | **392** | **173** |
| **Tanzania** | **583,245** | **57,637,628** | **885,803** | **44,579** | **1,293** | **5** |

### 7.2.2 Uwiano wa Askari na Ukubwa wa Eneo.

Pamoja na kuhudumia idadi kubwa ya watu, kila askari Polisi bado ana eneo kubwa la mraba la kuhudumia. Jedwali Na. 7.1 linaonesha kuwa Tanzania ina wastani wa askari 5 kwa kila kilomita 100 za mraba za kuhudumia. Hii inamaanisha kuwa, askari mmoja ana eneo la kilomita 19.5 za mraba za kuhudumia. Hata hivyo uwiano huo wa askari kwa eneo hutofautiana kati ya mkoa na mkoa.

Mikoa inayoongoza kuwa na uwiano mdogo wa askari kwa eneo la kilomita 100 za mraba ni Lindi, Katavi na Tabora (1 kwa kila mmoja), Songwe, Ruvuma, Manyara na Singida (2 kwa kila mmoja). Idadi ndogo ya uwiano wa askari inachangiwa na ukweli kuwa baadhi ya kilometa za mraba katika mikoa hii ni mapori, maeneo rasmi ya hifadhi za taifa na mbuga za wanyama. Mikoa yenye idadi kubwa ya uwino wa askari kwa eneo la kilomita 100 za mraba ni Dar es Salaam (522),Mjini Magharibi (173) na Kaskazini Unguja (92)

Hata hivyo, kuna askari hususan katika Makao Makuu ya mikoa na wilaya ambao hawashughuliki na uhalifu moja kwa moja bali hushughulika na kazi maalumu kama vile utawala, utaalamu, ufundi na ulinzi. Hali hii inapunguza idadi ya askari waliopo kushughulikia uhalifu moja kwa moja.

### 7.2.3 Idadi ya Makosa ya Jinai kwa Askari

Pamoja na idadi ya watu na eneo kwa kilometa za mraba, idadi ya makosa ya jinai yanayotokea katika jamii huchangia uzito wa kazi kwa askari polisi. Jedwali Na. 7.1 linabainisha kuwa askari mmoja anatakiwa kupeleleza wastani wa makosa 13 kwa mwaka. Idadi hii ya makosa hutofautiana baina ya mkoa na mkoa, ambapo Mwanza askari mmoja anatakiwa kupepeleleza makosa 26, Dar- es-Salaam (19), Geita na Kilimanjaro (19 kila moja) na Mbeya (16). Mikoa ya Tanzania Zanzibar ina uwiano mdogo zaidi wa makosa ya kuchunguzwa (2) kwa kila askari.

## 7.3 Makosa ya Usalama Barabarani

Mwaka 2020, Jeshi la Polisi lilikuwa na idadi ya askari 4,665 wa kikosi cha usalama barabarani ikilinganishwa na idadi ya askari 5,314 kwa mwaka 2019, sawa na upungufu wa askari 649. Takwimu zinaonesha kuwa, katika kipindi hicho kulikuwa na jumla ya makosa makubwa na madogo ya usalama barabarani 2,154,466. Makosa makubwa yalikuwa 1,933 (asilimia 0.1) ya makosa yote na makosa madogo yalikuwa 2,152,533 (asilimia 99.9). Hii ina maana kuwa askari mmoja alitakiwa kushughulikia makosa 462 ya usalama barabarani kwa mwaka 2020.

Jedwali Na.7.2 linatoa takwimu zinazoonesha uwiano wa makosa ya usalama barabarani kwa kila askari wa kikosi cha usalama barabarani. Uwiano huu unatofautiana baina ya mkoa na mkoa, ambapo mikoa yenye uwiano mkubwa ni Rufiji (1:777), Mwanza (1:692), Dar es Salaam (1:684 ),Pwani (632) na Tanga (1:629) Mikoa yenye uwiano mdogo ni Kusini Unguja (1:49), Mjini Magharibi (1:55).na Kusini Pemba (1:68).

**Jedwali Na. 7.2: Uwiano Kati ya Matukio ya Usalama Barabarani na Idadi ya Watu kwa Askari kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari - Desemba, 2020**

| Mkoa | Matukio ya Usalama Barabarani | Idadi ya Watu | Idadi ya Askari | Watu / Askari | Matukio / Askari |
|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 141,632 | 2,104,074 | 273 | 7,707 | 519 |
| Dar es Salaam | 506,642 | 5,401,814 | 741 | 7,290 | 684 |
| Dodoma | 96,430 | 2,647,410 | 240 | 11,031 | 402 |
| Geita | 59,919 | 2,434,800 | 116 | 20,990 | 517 |
| Iringa | 65,346 | 1,149,481 | 148 | 7,767 | 442 |
| Kagera | 59,373 | 3,238,347 | 144 | 22,489 | 412 |
| Katavi | 15,300 | 805,887 | 54 | 14,924 | 283 |
| Kigoma | 35,634 | 2,800,919 | 79 | 35,455 | 451 |
| Kilimanjaro | 99,411 | 1,951,252 | 159 | 12,272 | 625 |
| Lindi | 27,950 | 1,025,800 | 97 | 10,575 | 288 |
| Manyara | 26,585 | 1,672,386 | 119 | 14,054 | 223 |
| Mara | 40,024 | 1,873,105 | 97 | 19,310 | 413 |
| Mbeya | 85,522 | 2,204,543 | 187 | 11,789 | 457 |
| Morogoro | 80,967 | 2,730,058 | 305 | 8,951 | 265 |
| Mtwara | 25,986 | 1,478,874 | 100 | 14,789 | 260 |
| Mwanza | 128,092 | 3,826,573 | 185 | 20,684 | 692 |
| Njombe | 52,778 | 837,557 | 114 | 7,347 | 463 |
| Pwani | 138,373 | 749,580 | 219 | 3,423 | 632 |
| Rufiji | 42,742 | 576,272 | 55 | 10,478 | 777 |
| Rukwa | 36,619 | 1,270,049 | 90 | 14,112 | 407 |
| Ruvuma | 50,494 | 1,655,443 | 92 | 17,994 | 549 |
| Shinyanga | 55,461 | 1,993,589 | 109 | 18,290 | 509 |
| Simiyu | 19,155 | 2,304,228 | 81 | 28,447 | 236 |
| Singida | 58,526 | 1,705,182 | 135 | 12,631 | 434 |
| Songwe | 33,451 | 1,278,850 | 68 | 18,807 | 492 |
| Tabora | 46,944 | 3,081,263 | 178 | 17,310 | 264 |
| Tanga | 99,405 | 2,449,235 | 158 | 15,501 | 629 |
| Tarime – Rorya | 10,204 | 719,459 | 56 | 12,847 | 182 |
| **Tanzania Bara** | **2,138,965** | **55,966,030** | **4,399** | **12,722** | **486** |
| | | | | | |
| Kaskazini Unguja | 2401 | 232,480 | 35 | 6,642 | 69 |
| Kusini Unguja | 2193 | 138,589 | 45 | 3,080 | 49 |
| Mjini Magharibi | 7,150 | 733,914 | 131 | 5,602 | 55 |
| Kaskazini Pemba | 1527 | 294,267 | 22 | 13,376 | 69 |
| Kusini Pemba | 2230 | 272,348 | 33 | 8,253 | 68 |
| **Tanzania Zanzibar** | **15,501** | **1,671,598** | **266** | **6,284** | **58** |
| | | | | | |
| **Tanzania** | **2,154,466** | **57,637,628** | **4,665** | **12,355** | **462** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

# SURA YA NANE

# NGUVU KAZI YA JESHI LA POLISI

## 8.0 Utangulizi

Kufuatana na Sheria ya Jeshi la Polisi na Wasaidizi wa Polisi, Sura 322 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002, Tanzania inahitaji askari wenye ujuzi ili kuweza kutoa huduma iliyo bora kwa kutumia nguvu kazi. Sura hii inaangalia mabadiliko ya nguvu kazi katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020.

## 8.1 Nguvu Kazi ya Jeshi la Polisi, Tanzania

Jeshi la Polisi lina aina mbili za waajiriwa, askari Polisi na wafanyakazi raia. Hadi kufikia mwezi Desemba Jeshi la Polisi ukilinganisha na makisio ya idadi ya watu 57,637,628 kwa mwaka 2020 nchini ambayo inafanya askari mmoja kuhudumia watu 1,293,

Kwa kuzingatia majukumu ya Jeshi la Polisi ni muhimu kulinganisha nguvu kazi iliyopo na mahitaji ili kutoa huduma bora. Idadi ya askari inaweza kupungua kutokana na kustaafu, kuacha kazi, kufukuzwa, kuumwa au kufariki dunia. Mahitaji ya askari yanaweza kuongezeka kutokana na ukuaji wa uchumi, kuongezeka kwa matukio ya uhalifu na ongezeko la watu na makazi. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 jumla ya askari 1,194 waliondolewa kwenye ikama ya Jeshi la Polisi kutokana na sababu mbalimbali (Jedwali Na.8.1). Kwa maana hiyo inabidi hatua zichukuliwe kuziba pengo la askari hao.

**Jedwali Na. 8.1: Idadi ya Maafisa, Wakaguzi na Askari Walioacha Jeshi kwa Sababu Mbalimbali, Tanzania, Januari – Desemba, 2020**

| Sababu | Maafisa | Wakaguzi | Askari wa R&F | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kustaafu kwa lazima | 13 | 45 | 782 | 840 |
| Kustaafu kwa hiyari | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Kuacha kazi / Kununua mkataba | 0 | 5 | 11 | 16 |
| Utoro Jeshini | 0 | 1 | 62 | 63 |
| Vifo | 9 | 17 | 166 | 192 |
| Kufukuzwa kazi | 3 | 2 | 75 | 80 |
| Kumalizika kwa mkataba | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kuacha kazi kwa sababu ya ugonjwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kukoma kuwa na sifa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **27** | **70** | **1,097** | **1,194** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

Kama ilivyochambuliwa katika Sehemu ya 7.2.1, uwiano wa askari kwa idadi ya watu hapa nchini ni mkubwa kuliko kiwango cha 1:450 kinachopendekezwa kimataifa. Jedwali Na. 8.2 linaonesha uwiano kuanzia kipindi cha mwaka 2011 hadi 2020.

**Jedwali Na. 8.2: Nguvu Kazi na Mwelekeo wa Uwiano wa Askari kwa Idadi ya Watu, Tanzania, Januari – Desemba, 2011 - 2020**

| Mwaka | Kuacha Kazi kwa Kununua/ kumaliza Mkataba* | Kustaafu Kazi kwa Hiari au Lazima | Kuachishwa/Utoro | Vifo | Idadi ya Watu | Uwiano wa Askari kwa Watu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2011 | 82 | 272 | 117 | 167 | 44,476,500 | 1:1,214 |
| 2012 | 33 | 486 | 120 | 112 | 44,928,923 | 1:1,081 |
| 2013 | 12 | 285 | 158 | 145 | 46,158,529 | 1:1,115 |
| 2014 | 15 | 440 | 60 | 125 | 47,421,786 | 1:1,097 |
| 2015 | 53 | 415 | 130 | 126 | 48,719,617 | 1:1,071 |
| 2016 | 15 | 626 | 181 | 163 | 50,144,175 | 1:1,049 |
| 2017 | 20 | 620 | 220 | 113 | 51,557,365 | 1:1100 |
| 2019 | 3 | 648 | 186 | 194 | 54,199,168 | 1:1,182 |
| 2019 | 0 | 884 | 37 | 180 | 55,890,747 | 1:1,228 |
| 2020 | 12 | 842 | 143 | 192 | 57,637,628 | 1:1,293 |

*Inajumuisha kukoma kuwa na sifa
Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

Upungufu wa askari unachangiwa na mashambulizi yanayofanywa na wahalifu wakati wa kuwakamata au wakati wa doria, Ajali za Barabarani kwa askari kupata ajali wanapokuwa kwenye kazi au madereva kuwagonga askari pindi wanaposimamishwa kwenye vizuizi. Mara nyingine hutokea mapambano kati ya askari na wahalifu wanaokataa kujisalimisha au kutotii amri halali ya kukamatwa. Katika mazingira hayo vifo na majeruhi kwa askari hutokea (Jedwali Na. 8.3).

**Jedwali Na. 8.3: Idadi ya Askari Waliojeruhiwa na Waliokufa Wakiwa Kazini kwa Mikoa ya Kipolisi, Tanzania, Januari – Desemba, 2019 na 2020**

| | Askari Waliojeruhiwa | | Askari Waliokufa | |
|---|---|---|---|---|
| **Mkoa** | **2019** | **2020** | **2019** | **2020** |
| Arusha | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Dar-es-Salaam | 0 | 6 | 0 | 0 |
| Dodoma | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Geita | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Kigoma | 4 | 3 | 0 | 0 |
| Kilimanjaro | 0 | 8 | 0 | 1 |
| Kusini Unguja | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Lindi | 0 | 10 | 0 | 1 |
| Kusini Pemba | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Kaskazini Pemba | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Manyara | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Mara | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mbeya | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Morogoro | 0 | 1 | 0 | 3 |
| Mtwara | 0 | 3 | 0 | 2 |
| Mwanza | 3 | 2 | 0 | 0 |
| Njombe | 0 | 9 | 0 | 4 |
| Pwani | 1 | 5 | 0 | 0 |
| Rufiji | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Rukwa | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Ruvuma | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Shinyanga | 0 | 8 | 0 | 0 |
| Songwe | 0 | 10 | 0 | 1 |
| Tabora | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Tanga | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Tarime/Rorya | 8 | 4 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **18** | **89** | **0** | **13** |

Chanzo: Jeshi la Polisi Tanzania

*Angalizo: mikoa ambayo haipo kwenye jedwali haikuwa na Askari waliojeruhiwa au kufariki kwa miaka ya 2019 hadi 2020*

# SURA YA TISA

## MKAKATI WA KUKABILIANA NA UHALIFU

### 9.0 Utangulizi

Mkakati wa kudhibiti na kukabiliana na uhalifu nchini unatokana na uchambuzi wa kina wa makosa ya jinai na usalama barabarani yaliyo ripotiwa. Sura hii inaonesha aina ya makosa, vyanzo na changamoto za hali ya uhalifu nchini pamoja na mikakati ya kukabiliana na hali ya uhalifu kwa mwaka 2020. Takwimu hizi ni muhimu katika kuandaa mipango ya kudhibiti na namna ya kupambana na uhalifu, kwa kuainisha na kuanzisha mikakati mipya, kuboresha mikakati iliyopo pamoja na kupata rasilimali za kutosha kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kutokomeza uhalifu na kupunguza ajali za barabarani nchini.

Takwimu ambazo zimekuwa zikiripotiwa zimetumika kuelezea mikakati mbambali dhidi ya makosa yafuatayo:

i. Makosa dhidi ya binadamu;
ii. Makosa ya kuwania mali;
iii. Makosa dhidi ya maadili ya jamii;
iv. Matukio ya usalama barabarani;
v. Makosa ya uhalifu wa kifedha; na
vi. Makosa kwa njia ya mtandao.

Mikakati ya kudhibiti na kupambana na makosa mbalimbali imeelezwa kwa muhtasari kwenye majedwali yafuatayo:

## 9.1 Makosa Dhidi ya Binadamu

**Jedwali Na. 9.1: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa Dhidi ya Binadamu, Tanzania, 2020**

| **Makosa Dhidi ya Binadamu** | | | |
|---|---|---|---|
| **Kosa** | **Idadi ya Makosa (Januari - Desemba, 2020 )** | **Chanzo** | **Mikakati** |
| 1. Mauaji | 2,225 | i. Imani za kishirikina.<br>ii. Visasi.<br>iii. Tamaa ya kupata mali kinyume cha sheria.<br>iv. Ulevi wa kupindukia.<br>v. Wivu wa mapenzi/ugoni.<br>vi. Migogoro ya ardhi/mali. | i. Kuhamasisha jamii kuachana na vitendo vya kushiriki kwenye mauaji ya wazee, albino au mtu yeyote anayekabiliwa na tuhuma zinazohusiana na masuala ya jinai.<br>ii. Kutoa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali ili jamii ibadilike na kuacha kujichukulia sheria mkononi.<br>iii. Kuendelea kuimarisha kikosi maalumu cha kupambana na matukio ya mauaji.<br>iv. Kuhamasisha jamii ili ijihusishe na shughuli zilizo halali katika kujipatia kipato.<br>v. Jeshi la Polisi kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya Ardhi.<br>vi. Kushirikisha Taasisi za kidini katika kuhamasisha jamii ili kuachana na imani potofu. |
| 2. Kubaka | 7,263 | i. Utandawazi<br>ii. Imani za kishirikina<br>iii. Tamaa za kimwili<br>iv. Kukosa maadili ya kidini na kijamii. | i. Kuendelea kuielimisha jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika usimamizi wa sheria ipasavyo (Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya Mwaka 2019).<br>ii. Kuelimisha jamii kuzingatia na kufuata maadili ya Kitanzania.<br>iii. Kushirikisha Taasisi nyingine zikiwemo za kidini katika kuhamasisha jamii ili kuachana na imani potofu za kishirikina.<br>iv. Kushirikiana na wadau wengine ikiwemo Idara ya Uhamiaji katika kudhibiti biashara haramu ya kusafirisha binadamu. |
| 3. Kunajisi | 52 | | |
| 4. Kulawiti | 1,205 | | |
| 5. Kutupa Watoto | 153 | i. Matatizo ya kiuchumi.<br>ii. Ugonjwa wa akili.<br>iii. Hofu ya kutengwa ama kutelekezwa na familia. | |
| 6. Wizi wa Watoto | 84 | i. Ugumba.<br>ii. Imani ya kishirikina. | |
| 7. Usafirishaji haramu wa Binadamu | 19 | Tamaa ya kujipatia kipato kikubwa. | |

## 9.2 Makosa ya Kuwania Mali

**Jedwali Na. 9.2: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa ya Kuwania Mali, Tanzania, 2020**

<table>
<tr><th colspan="4">Makosa ya Kuwania Mali</th></tr>
<tr><th>Kosa</th><th>Idadi ya Makosa (Januari - Desemba, 2020 )</th><th>Chanzo</th><th>Mikakati</th></tr>
<tr><td>1. Unyang’anyi wa Kutumia Silaha</td><td>297</td><td rowspan="8">i. Hali duni ya kiuchumi.<br>ii. Kukosa maadili.<br>iii. Ukuaji wa miji.<br>iv. Utandawazi.<br>v. Tofauti kubwa ya hali ya maisha kati ya walionacho na wasionacho.<br>vi. Ukosefu wa ajira kwa vijana.<br>vii. Tamaa ya kumiliki mali.</td><td rowspan="8">i. Kuhamasisha jamii hasa vijana kushiriki katika shughuli halali za ujasiriamali/uchumi ili kujipatia kipato.<br>ii. Kuzishawishi taasisi za fedha ili ziweze kupunguza urasimu wa upatikanaji wa mikopo na kupunguza riba kubwa zinazotozwa katika mikopo hiyo.<br>iii. Kuwepo na mipango endelevu ya utoaji elimu kwa umma hasa elimu ya ujasiriamali.<br>iv. Kuhamasisha jamii ijenge utamaduni na utaratibu wa kutoa taarifa kwa wakati kwenye vyombo vya dola wanapobaini viashiria vya uhalifu.</td></tr>
<tr><td>2. Unyang’anyi wa Kutumia Nguvu</td><td>1,482</td></tr>
<tr><td>3. Uvunjaji</td><td>12,486</td></tr>
<tr><td>4. Wizi</td><td>87</td></tr>
<tr><td>5. Wizi wa Pikipiki</td><td>4,823</td></tr>
<tr><td>6. Wizi wa Magari</td><td>175</td></tr>
<tr><td>7. Wizi wa Mifugo</td><td>3,707</td></tr>
<tr><td>8. Kuchoma Nyumba Moto</td><td>982</td></tr>
</table>

## 9.3 Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii

**Jedwali Na. 9.3: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii, Tanzania, 2020.**

<table>
<tr><th colspan="4">Makosa Dhidi ya Maadili</th></tr>
<tr><th>Kosa</th><th>Idadi ya Makosa (Januari - Desemba 2020)</th><th>Chanzo</th><th>Mikakati</th></tr>
<tr><td>1. Kupatikana na Silaha</td><td>169</td><td rowspan="8">i. Hali duni ya kiuchumi<br>ii. Ujangili<br>iii. Tamaa ya kujipatia mali.<br>iv. Migogoro ya kisiasa katika baadhi ya nchi za jirani.<br>v. Tamaa za kujipatia kipato kwa njia isiyo halali.<br>vi. Kukosa maadili<br>vii. Sababu za kimazingira na makundi mabaya.<br>viii. Upungufu wa ajira<br>ix. Tamaa (kipato na mali)</td><td rowspan="8">i. Kuendelea kushirikiana na jamii kutumia falsafa ya polisi jamii ili kushirikiana katika mapambano dhidi ya wahalifu.<br>ii. Kushirikiana na wadau mbalimbali kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mipaka ili kubaini wageni wanaoingia na kutoka nchini.<br>iii. Kushirikiana na nchi jirani kufanya operesheni ya pamoja na misako ya wahalifu ndani na nje ya nchi<br>iv. Kuelimisha jamii na wadau wengine juu ya athari za dawa za kulevya<br>v. Kuwahamasisha vijana kushiriki katika shughuli za kijamii na kiutamaduni<br>vi. Kuendeleza operesheni na misako ya kuwakamata wanaojihusisha na uuzaji au utumiaji wa dawa za kulevya.<br>vii. Kushirikisha wazazi na walezi katika ngazi ya familia, shule na vyuo kwa kutoa elimu na mafunzo ya maadili na ya uraia.<br>viii. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira ili kutunza na kuhifadhi rasilimali za nchi yetu<br>ix. Kuendelea kuwapatia mafunzo askari wanaopita katika vyuo vya polisi juu ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya<br>x. Kuelimisha jamii kuhusu madhara yatokanayo na rushwa.<br>xi. Hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wale watakaokamatwa kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa</td></tr>
<tr><td>2. Kupatikana na Dawa za kulevya za viwandani</td><td>429</td></tr>
<tr><td>3. Kupatikana na Bhangi</td><td>5,903</td></tr>
<tr><td>4. Kupatikana na Mirungi</td><td>1,031</td></tr>
<tr><td>5. Kupatikana na Nyara za Serikali</td><td>728</td></tr>
<tr><td>6. Kupatikana na Pombe Haramu ya Moshi</td><td>4,602</td></tr>
<tr><td>7. Wahamiaji Haramu</td><td>862</td></tr>
<tr><td>8. Rushwa</td><td>3</td></tr>
</table>

## 9.4 Makosa ya Uhalifu wa Kifedha

**Jedwali Na. 9.4: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa ya Utakatishaji Fedha, Tanzania, 2020**

<table>
<tr><th colspan="4">Makosa ya Uhalifu wa Kifedha</th></tr>
<tr><th>Kosa</th><th>Idadi ya Makosa (Januari - Desemba, 2020)</th><th>Chanzo</th><th>Mikakati</th></tr>
<tr><td>1. Kupatikana na Noti Bandia.</td><td>78</td><td rowspan="7">i. Hali duni ya kiuchumi<br>ii. Kukosa maadili<br>iii. Ukuaji wa miji<br>iv. Utandawazi<br>v. Umaskini<br>vi. Tofauti kubwa ya hali ya maisha kati ya walionacho na wasionacho<br>vii. Ukosefu wa ajira kwa vijana<br>viii. Tamaa ya mali</td><td rowspan="7">i. Kuhamasisha jamii hasa vijana kushiriki katika shughuli za ujasiriamali<br>ii. Kuzishawishi taasisi za fedha kupunguza urasimu wa upatikanaji wa mikopo na kupunguza riba kubwa zinazotozwa kwa mikopo hiyo<br>iii. Kuwepo na mipango ya utoaji elimu kwa jamii hasa ya elimu ya ujasiriamali<br>iv. Kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kusimamia maadili ya jamii<br>v. Kuendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi kufuata maadili ya kazi, kanuni, taratibu na sheria kwa kuzingatia viapo vyao</td></tr>
<tr><td>2. Kughushi.</td><td>744</td></tr>
<tr><td>3. Wizi katika Mabenki.</td><td>0</td></tr>
<tr><td>4. Wizi katika Serikali Kuu</td><td>23</td></tr>
<tr><td>5. Wizi katika Serikali za Mitaa</td><td>6</td></tr>
<tr><td>6. Wizi katika Vyama vya Ushirika</td><td>4</td></tr>
<tr><td>7. Wizi katika Mashirika ya Umma.</td><td>50</td></tr>
</table>

## 9.5 Makosa kwa Njia ya Mtandao

**Jedwali Na. 9.5: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa kwa Njia ya Mtandao, Tanzania, 2020**

| Makosa ya Mtandao | | | |
|---|---|---|---|
| **Kosa** | **Idadi ya Makosa (Januari - Desemba, 2020 )** | **Chanzo** | **Mikakati** |
| 1. Wizi katika ATM | 53 | i. Hali duni ya kiuchumi.<br>ii. Kukosa maadili.<br>iii. Ukuaji wa miji<br>iv. Tamaa ya kujipatia mali.<br>v. Utandawazi.<br>vi. Tofauti kubwa ya hali ya maisha kati ya walionacho na wasionacho.<br>vii. Ukosefu wa ajira kwa vijana.<br>viii. Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. | i. Kuhamasisha vijana kushiriki katika ujasiriamali.<br>ii. Kuzishawishi taasisi za fedha kupunguza urasimu wa upatikanaji wa mikopo na kupunguza riba kubwa zinazotozwa kwa mikopo hiyo.<br>iii. Kuwepo na mipango ya utoaji elimu kwa umma hasa elimu ya ujasiriamali.<br>iv. Kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kusimamia maadili ya jamii.<br>v. Kuelimisha watumiaji wa mitandao juu ya usiri wa nywila (neno la siri) zao na umuhimu wa kutomwamini mtu kuhusu nywila zao.<br>vi. Kuendelea kutoa elimu ya sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka, 2019<br>vii. Kufanya doria za mtandaoni |
| 2. Wizi kupitia huduma za fedha, kupitia simu za mkononi (Mpesa, Tigo pesa na Airtel money n.k) | 2,963 | | |
| 3 Makosa ya jinai yanayohusisha matumizi mabaya ya mtandao (matusi, unyanganyi wa kutumia silaha, mauaji, kutakatisha fedha, mwizi akiwa mtumishi, kubaka, uchochezi, utapeli, vitisho, ujangili na matumizi mabaya ya mtandao) | 1,834 | | |

## 9.6 Matukio ya Ajali za Barabarani

**Jedwali Na. 9.6: Mikakati Inayotumika Kudhibiti na Kupambana na Makosa ya Ajali za Barabarani, Tanzania, 2020**

| Matukio ya Ajali za Barabarani | | | |
|---|---|---|---|
| **Kosa** | **Idadi ya Makosa (Januari - Desemba, 2020)** | **Chanzo** | **Mikakati** |
| 1. Ajali za barabarani | 1,933 | i. Ukosefu wa elimu kwa baadhi ya watumiaji wa vyombo vya moto.<br>ii. Kutofuata sheria za barabarani kama vile kuendesha kwa mwendo kasi<br>iii. Kutofuata matumizi sahihi ya alama za barabarani kwa watumiaji wa barabara<br>iv. Uchakavu wa vyombo vya usafiri<br>v. Ubovu wa miundombinu.<br>vi. Ulevi.<br>vii. Uzembe. | i. Kuongeza idadi ya askari wa kikosi cha usalama barabarani.<br>ii. Kudhibiti mwendo kasi kwa kuweka vituo vya ukaguzi wa ratiba za magari ya abiria.<br>iii. Kuimarisha doria na ukaguzi katika barabara kuu.<br>iv. Kutoa adhabu stahiki na rekebishi kwa wakosaji.<br>v. Kusimamia utaratibu wa kuondoa pointi za sifa za udereva kwa kila kosa na hatimaye kumfutia leseni dereva.<br>vi. Kuendelea kutoa elimu ya usalama barabarani kupitia vipindi vya redio na televisheni, pamoja na kuelimisha wakosaji inapobidi kwa kutumia vipeperushi.<br>vii. Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha kuwa wamiliki wa vyombo vya usafiri wanaajiri watu wenye ujuzi na sifa za kuwa madereva ili kuweza kupunguza ajali zinazoweza kuepukika na zinazosababisha uharibifu wa vyombo, vifo na majeruhi.<br>viii. Ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri. |
| 2. Ajali zilizosababisha vifo | 1,031 | | |
| 3. Ajali zilizosababisha majeruhi | 646 | | |
| 4. Ajali za kawaida | 256 | | |
| 5. Watu waliokufa | 1,384 | | |
| 6. Watu waliojeruhiwa | 2,362 | | |

# SURA YA KUMI

## MATUKIO YALIYOVUTA HISIA KWA JAMII

### 10.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea matukio ya uhalifu yaliyovuta hisia katika jamii. Matukio haya ni yale ambayo kutokea kwake husababisha mshtuko kwa jamii na kwamba si kawaida jambo hilo kutokea.

### 10.1 Matukio ya Kushtua Yaliyotokea Januari - Desemba, 2019

Yafuatayo ni baadhi ya matukio ya kushtua ambayo yalivuta hisia kwa jamii katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2019 kama yalivyoripotiwa kutoka sehemu mbalimbali nchini.

**1. KILIMANJARO**

**MAUAJI**

Mnamo tarehe 01.02.2020 Majira ya saa 20:00 huko Majengo eneo la Uwanja wa mpira wa miguu Kata ya Majengo Tarafa ya Moshi Mashariki (W) Moshi. Jumla ya watu ishirini (20) kati yao watoto 5 wanawake 14 na mwanaume mmoja walifariki kwa kukanyagwa na wenzao wakati wanakimbilia kukanyaga mafuta ya upako yaliyokuwa yamewekwa getini na Askofu Boniphace Mwamposa na wenzake. Awali, Askofu Boniphace Mwamposa aliomba kibali cha kufanya mkutano wa injili kuanzia tarehe 30.01.2020 mpaka tarehe 01.02.2020 muda kuanzia saa 06:00 asubuhi mpaka saa 18:00. Tarehe 01.02.2020 ilikuwa ni siku ya mwisho ambapo askofu alipitiliza muda na ilipofika majira ya saa 19:30hrs ndipo alipowaambia waumini wake wapite kwenye mafuta yaliyokuwa yamemwagwa kwenye turubai getini ndipo yalipotokea maafa. Askofu Boniphace s/o Mwamposa alitoroka baada ya tukio hilo na alikamatwa baadae.

**2. NJOMBE.**

**AJALI YA GARI KUGONGA MAGARI MAWILI NA KUSABABISHA VIFO NA MAJERUHI**

Mnamo tarehe 03.02.2020 majira ya 06:10 asubuhi huko barabara ya Njombe/ Songea eneo la Mlima wa NBC/Polisi Njombe Kata ya Njombe Mjini (W) Njombe, gari lenye namba T 349 CXB aina ya Yutong bus mali ya kampuni ya Sharon ya Arusha lililigonga gari namba PT 3734 aina ya Toyota Landcruiser lililokuwa linawapeleka askari kazini na kusababisha vifo kwa askari watatu na majeruhi 8. Chanzo ni uzembe wa dereva wa basi kujaribu kulipita gari lingine bila kuchukua tahadhari.

**3. LINDI**

**TAARIFA YA MAFURIKO**

Mnamo tarehe 26.01.2020 majira 01:00 usiku katika kata ya Njinjo Wilaya ya Kilwa, kulitokea mafuriko makubwa yaliyosababisha maafa baada ya mto Matandu kujaa maji yaliyosababishwa na kunyesha kwa mvua kubwa. Aidha, mafuriko hayo yameathiri nyumba za makazi ya watu zaidi ya 1,000, mashamba na mifugo. Katika tukio hilo Kamati ya maafa wilaya ya Kilwa na kikosi cha CRT Kilwa walifika katika kijiji hicho cha Njinjo na kusaidiana na waokoaji wa kijiji kuokoa watu waliokuwa wamezingirwa na maji katika vijiji vyao wakiwa na boti moja na kufanikiwa kuokoa watu zaidi ya 400 wengi wao wakiwa ni watoto na wazee na kuhifadhiwa katika shule ya msingi Kipindimbi.

**4. MOROGORO**

**KUFANYA KITENDO KINACHOUMIZA HISIA ZA WAUMINI WA DINI YA KIISLAMU**

Mnamo tarehe 06.02.2020 majira ya 14:50 huko eneo la Uhindini, Kata ya Kasiki, Tarafa ya Kilosa Mjini, Wilaya ya Kilosa, mtu mmoja mwanaume, alichana na kuchoma moto kitabu cha dini ya kiislamu kiitwacho ‘’Juzzu Amma’’ kitendo ambacho kiliibua hisia kali kwa kuwakasirisha waumini wa dini ya kiislamu. Mtuhumiwa alikamatwa kwa hatua za kisheria.

**5. RUFIJI**

**KUCHOMA NYUMBA MOTO NA KUSABABISHA VIFO**

Mnamo tarehe 08.02.2020 majira kati ya 02:30 - 03:00 usiku huko katika Kitongoji cha Uponda chini Kijiji cha Uponda kata ya Mjawa, Tarafa ya Kibiti (W) Kibiti, mwanamme mmoja alichoma nyumba ya mpenzi /hawara yake na kusababisha vifo vya watu sita. Eneo la tukio kumekutwa ndoo ya Lita 10 ikiwa na masalia ya mafuta ya petrol kiasi cha lita moja ambayo yanasadikiwa/inaaminika kutumika kufanya uhalifu huo. Mbinu iliyotumika ni kufunga milango ya nyumba kwa nje, kumwanga petrol kisha kuchoma moto. Chanzo ni wivu wa kimapenzi.

**6. TEMEKE**

**WIZI**

Mnamo tarehe 07.02.20 majira ya saa 17.30 huko maeneo ya Chang'ombe karibu na kituo cha kuwekea mafuta cha Camel oil lilionekana gari namba T.728 BAN aina ya Nissani mali ya kampuni ya ulinzi ya G4S ikiwa imetelekezwa na ndani ya gari zilikuwamo silaha mbili, moja aina ya pump action shotgun yenye no TZCAR 92504 na nyingine pistol iliyofungiwa ndani ya gari. Awali, gari hiyo ilikuwa na dereva na walinzi wawili ambao walikuwa wanasindikiza pesa kiasi cha Tshs 1,300,000,000/= na USD 500,000/= mali ya bank ya NBC kutoka tawi la Samora kwenda Posta Makao Makuu ya NBC Bank na kisha kutokomea kusikojulikana. Watuhumiwa wote walifanikiwa kukamatwa wakiwa na fedha pamoja na mali ambazo tayari walishazinunua kutokana na fedha walizoziiba.

**7. TANGA**

**AJALI YA MABEHEWA YA TRENI KUGONGANA NA KIBERENGE NA KUSABABISHA VIFO VYA WATU 5 NA MAJERUHI 1**.

Mnamo tarehe 19.03.2020 Treni ya mizigo iliyokuwa inatoka Tanga kuelekea Ruvu Mkoani Pwani, ilipata ajali huko maeneo ya kitongoji cha Mgongola "B" kijiji cha Kwadoya kata ya Kwamgwe tarafa ya Mkumburu (W) Handeni ambapo mabehewa matano yaliacha njia na kupinduka. Mnamo tarehe 22/03/2020, Shirika la Reli Tanzania (TRC) waliamua kufanya kazi ya kushusha mzigo wa cement toka kwenye mabehewa yaliyokuwa yamepinduka tarehe 19.03.2020 kuyaweka kwenye mabehewa mazima kwa ajili ya mzigo huo kusafirishwa kwenda Ruvu baada ya kumaliza kuyaweka relini mabehewa hayo yalianza kutembea/kukimbia yenyewe bila ya engine na yalipofika kitongoji cha Mgongola "A" kijiji cha Kwadoya kata ya Kwamgwe tarafa ya Mkumburu (W) Handeni yalikuta Kiberenge kilichokuwa na wafanyakazi sita. Kiberenge hicho kiligongwa na mabehewa matatu na kusababisha vifo vya wafanyakazi watano na majeruhi mmoja.

**8. SHINYANGA**

**KUPATIKANA NA NYARA ZA SERIKALI.**

Mnamo tarehe 03.05.2020 majira ya 23:45 huko mtaa wa Lubaga, kata ya Lubaga Mmanispaa ya Shinyanga Jeshi la Polisi mkoa wa Shiyanga likishirikiana na Maafisa wa wanyamapori mkoa wa Shinyanga walifanya upekuzi kwenye makazi ya Mh.Suleiman Masoud Suleiman, Mbunge wa Kishapu na kufanikiwa kukamata kg 35 za nyama ya swala ikiwa kwenye jokofu jikoni na kwenye 'frizer' iliyokuwa kwenye ukumbi wa mazoezi, nyama nyingine ilipatikana kwenye gari T760 DSD NISSAN hardbody iliyokuwa imeegeshwa ndani ya uzio wa nyumba hiyo na pia zilipatikana silaha

mbalimbali 15 na risasi 536 ambazo utunzaji wake ulikuwa ni hatarishi kwani zilitunzwa kwenye kabati la nguo na nyingine zikiwa hazina kibali cha kumiliki.

**9. KIGOMA**

**AJALI YA BOTI KUZAMA NDANI YA ZIWA NA KUSABABISHA VIFO VYA WATU 9.**

Mnamo tarehe 25.06.2020 majira ya 07:30 asubuhi huko maeneo ya Rasini katika Ziwa Tanganyika kijiji cha Sibwesa kata ya Kalya tarafa ya Buhingu wilaya ya Uvinza mkoa wa Kigoma, boti linalojulikana kwa jina la MV Nzeimana, ikiwa safarini kuelekea Ikola mkoa wa Katavi ikiwa na abiria wapatao 60 ilipata ajali ya kuzama Ziwani. Watu 9 walifariki kati yao wanawake 7 na wanaume 2. Watu 51 waliokolewa wakiwa hai.

**10. IRINGA**

**AJALI YA GARI KUPINDUKA NA KUSABABISHA VIFO VYA WATU 9 NA MAJERUHI 12.**

Tarehe 27.06.2020 majira ya 14:30 huko katika barabara kuu ya Iringa - Morogoro maeneo ya Mlima Kitonga kata ya Ilula na tarafa ya Mazombe wilaya ya Kilolo na mkoa Iringa, Gari no. T326 CSX aina ya Yutong bus linalofanya safari za Iringa – Dar Es Salaam likiwa linatokea Iringa kuelekea Dar Es Salaam liliacha barabara na kupinduka kisha kusababisha vifo vya abiria 9 na majeruhi 12. Chanzo cha ajali ni mwendokasi wa basi.

**11. KINONDONI**

**AJALI YA MOTO.**

Mnamo tarehe 17.07.2020 majira ya 15:30, Shule ya Kinondoni Muslim iliyopo mtaa wa Kinondoni Shamba, iliwaka moto na kuteketeza jumla ya vyumba 19 vya madarasa na mabweni 3 sambamba na baadhi ya magodoro na masanduku ya wanafunzi.

**12. TABORA**

**MAUAJI.**

Mnamo tarehe 06.09.2020 majira ya saa 17:30 huko katika Kitongoji cha Wachawaseme tarafa ya Igagala wilaya ya Kaliua waliuawa watu 8 na miili yao kuchomwa moto na kuteketea. Watuhumiwa 6 wamekamatwa.

## 13. TEMEKE

### KUSAFIRISHA DAWA ZA KULEVYA AINA YA HEROINE.

Mnamo tarehe 08.09.2020 majira ya saa 20:20 hivi huko maeneo ya Temeke Vertenary, walikamatwa watuhumiwa 4 wakiwa na dawa za kulevya aina ya Heroine zenye uzito wa kilogramu 51 pamoja na pesa taslimu Tsh 58, 000,000. Watuhumiwa wote wamafikishwa mahakamani.

## 14. KAGERA

### AJALI YA BWENI KUUNGUA MOTO NA KUSABABISHA VIFO VYA WANAFUNZI 10 NA MAJERUHI 7.

Mnamo tarehe 13.09.2020 majira ya 23:45 huko katika Shule ya Msingi Byamungu English Medium, Bweni moja la wanafunzi wa kiume lenye wanafunzi 74 wa madarasa kuanzia la kwanza hadi la sita liliungua moto na kusababisha vifo vya wanafunzi 10 na majeruhi 7. Chanzo cha ajali hiyo ni hitilafu ya mfumo wa nishati ya umeme jua.

## 15. KASKAZINI PEMBA

### SHAMBULIO LA KUDHURU MWILI.

Mnamo tarehe 22.09.2020 Majira ya saa 05.10 alfajiri huko katika Kata ya Kangagani Wilaya ya Wete mfuasi wa Chama cha ACT WAZALENDO aliingia katika Msikiti wa Kangagani na panga na kuwajeruhi watu wawili akiwemo Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa kata ya Kangagani. Chanzo cha tukio ni muhemuko wa kisiasa. Mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa mahakamani.

# SURA YA KUMI NA MOJA

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 11.0 Utangulizi

Baada ya kuangalia hali halisi ya uhalifu nchini kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 mapendekezo yametolewa ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi katika kufikia malengo ya kulinda amani, raia na mali zao pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi. Hii itasaidia kujenga mazingira salama kwa wananchi, taasisi na wawekezaji katika uzalishaji mali, shughuli za kijamii na ujenzi wa taifa kwa ujumla.

### 11.1 Hitimisho

Taarifa hii imeangalia hali ya uhalifu katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2020 na kulinganisha na miaka mitano iliyopita. Jeshi limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje pamoja na jamii kwa ujumla katika kupambana na uhalifu nchini. Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, 2020, uhalifu kwa Makosa Makubwa ya jinai ulipungua kwa asilimia 2.5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2019. Kwa upande wa usalama barabarani, matukio makubwa yalipungua kwa asilimia 26.7 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2019. Katika kutekeleza majukumu yake, Jeshi la Polisi limepata mafanikio pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza wajibu wake kwa uwazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na uwajibikaji. Hivyo basi, Jeshi la Polisi litaendelea kuhamasisha na kushirikisha taasisi mbalimbali, wadau na jamii kwa ujumla katika kutatua changamoto zitakazojitokeza. Ni matarajio kuwa Serikali itaendelea kulisaidia Jeshi la Polisi katika kutatua changamoto mbalimbali zilizopo ili kuongeza ufanisi katika kupambana na uhalifu nchini.

### 11.2 Mapendekezo

Ili kukabiliana na changamoto zilizopo katika kupambana na uhalifu, Jeshi la Polisi linatoa mapendekezo yafuatayo kwa Serikali na wadau:

i. Askari Polisi wajengewe uwezo na mbinu za kisasa zinazoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia hususan mbinu za uhalifu/wahalifu.
ii. Ikama iboreshwe na iendane na wakati na mazingira ya kazi ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka na changamoto zake.

iii. Kitengo cha Takwimu cha Jeshi la Polisi kiimarishwe na kujengewa uwezo na vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji katika mikoa na wilaya pamoja na kufanya tafiti maalum zinazohusiana na aina mbalimbali za uhalifu na wahalifu.

iv. Kuongezewa vitendea kazi hususan magari, pikipiki na vifaa vya kisasa vya upelelezi kwa Jeshi la Polisi nchini

v. Bajeti ya Jeshi la Polisi iongezwe ili iweze kukidhi mahitaji ambayo yatawezesha utendaji makini na huduma bora kwa wananchi katika kufanikisha dhana ya usalama na ulinzi shirikishi ili kujenga uchumi imara wa Viwanda kwa maendeleo ya nchi na watu wake.

vi. Kuendelea kutoa elimu ya uraia na uzalendo kwa wananchi ili waweze kutii sheria bila ya shuruti.

vii. Jeshi la Polisi liendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika ujenzi wa nyumba za makazi ya askari na vituo vya Polisi.

## Kiambatisho Na. 1

**Bajeti (TZS) ya Jeshi la Polisi Tanzania, 2015 - 2021** .

| Ainaya Matumizi | 2015 /16 | 2016 /17 | 2017 /18 | 2018 /19 | 2019/20 | 2020/221 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mengineyo** | 171,318,024,000 | 187,429,446,000 | 254,194,348,000 | 256,194,348,000 | 249,043,548,000 | 244,089,548,000 |
| **Maendeleo** | 5,010,968,000 | 5,370,041,105 | 5,253,623,000 | 3,749,851,000 | 2,792,924,679 | 2,034,050,000 |
| **Mishahara/PE** | 284,314,668,000 | 342,411,819,000 | 339,018,249,000 | 336,694,269,00 | 352,445,632,000 | 318,407,712,000 |